KUCHUNGUZA TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA NGANO ZA JAMII YA WANYAMWEZI

NEEMA USWEGE MWAKILA

TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2017

UTHIBITISHO

Aliyetia saini yake hapa chini, anathibitisha kuwa, amesoma tasnifu hii iitwayo **Kuchunguza Taswira ya Mwanamke katika Ngano za Jamii ya Wanyamwezi** na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya masharti ya kutunukiwa Digrii ya Uzamili (M.A) Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

.....

Dkt. Mohamed Omary

(Msimamizi)

Tarehe.....

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO

Mimi, **Neema Uswege Mwakila** nathibitisha kuwa tasinifu hii iitwayo ***Kuchunguza Taswira ya Mwanamke katika Ngano za Jamii ya Wanyamwezi*** ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

Sahihi

Tarehe

TABARUKU

Naitabaruku kazi yangu kwa wazazi wangu wapenzi Uswege Ambokile Mwakila na Catherine Yesaya Mwakila.

SHUKURANI

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uhai na afya njema na siha kwa kuniwezesha katika kipindi chote cha masomo yangu kwa na kunijaalia maarifa ambayo nimeweza kuyatumia katika kukamilisha masomo yangu ya Shahada ya Uzamili kwa kusema Nakushukuru sana Mungu Baba.

Pili, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu Daktari, Mohamed Omary kwa kunifuatilia kwa ukaribu sana na kuniongoza vyema kwa kila hatua ya utafiti huu bila kusita wala kuchoka kunishauri na kuniongoza kufanya marekebisho ya kazi hii hatua kwa hatua hadi ilipokamilika. Aidha, msaada wake ndio ulionifikisha katika hatua hii ya kukamilisha masomo yangu kwa ngazi hii, kwa hivyo Mungu ampe maisha marefu na afya njema kwani wapo watu wengi wanaohitaji msaada wake.

Tatu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wazazi wangu kwa kunilea na kunipeleka shule kwa lengo la kupata maarifa yanayonisaidia hadi kufikia leo hii. Pia, shukrani za pekee zimwendee mume wangu Paul Paschol Moke na watoto wangu Nyakubhoga Moke na Baraka Moke pamoja mjukuu wangu Audrey na mama yangu Catherine Yesaya Mwakila kwa uvumilivu wao wakati wa masomo pamoja na kunipa msaada ulioweza kufanikisha masomo yangu.

Nne, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wangu Profesa Emmanuel Mbogo, Profesa Tigiti Sengo na Daktari Peter Lipembe kwa kunipa maarifa ambayo yamenisaidia katika kufanikisha tasnifu hii. Mwenyenzi Mungu awape kila la kheri.

Asanteni Sana

IKISIRI

Mada ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza Taswira ya mwanamke katika Ngano za Jamii ya Wanyamwezi. Lengo kuu la utafiti lilifungamana na mada ya utafiti huku malengo ya utafiti yakiwa ni kuchambua taswira ya mwanamke katika ngano za Wanyamwezi na kuelezea uhalisia wa taswira ya mwanamke katika ngano za Wanyamwezi kwa jamii ya leo. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili na upitiaji wa nyaraka na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Ufeministi. Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa ngano za jamii ya Wanyamwezi zinamsawiri mwanamke kwa namna mbalimbali. Mwanamke anasawiriwa kama kiumbe katili, mwanamke ni kiumbe asiyependa watoto wa kambo, mwenye nguvu na akili nyingi, kutoshirikishwa katika maamuzi, mtu mwenye huruma, mtu mwenye busara na hekima na kiumbe mwema. Taswira hii ya mwanamke inayojitokeza katika ngano za jamii ya Wanayamwezi zina uhalisia katika maisha ya leo kwani wapo wanawake ambao wana tabia na mwenendo wa aina hii. Wapo wanawake wema na wapo wengine ambao ni waovu.

YALIYOMO

UTHIBITISHO ..... **ii**

HAKIMILIKI ..... **iii**

TAMKO ..... **iv**

TABARUKU ..... **v**

SHUKURANI ..... **vi**

IKISIRI ..... **vii**

SURA YA KWANZA **1**

1.0 UTANGULIZI **1**

1.1 Usuli wa Tamko la Utafiti 1

1.2 Tatizo la Utafiti 3

1.3 Malengo ya Utafiti 4

1.3.1 Lengo Kuu 4

1.4 Maswali ya Utafiti 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti 4

1.6 Mipaka ya Utafiti 6

1.7 Mpangilio wa Tasinifu 6

SURA YA PILI **7**

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA **7**

2.1 Utangulizi 7

2.2 Fasili ya Fasihi Simulizi 7

2.3 Ngano Kama Utanzu wa Fasihi Simulizi 8

2.4 Usawiri wa Mwanamke katika Fasihi Simulizi kwa Ujumla 12

2.5 Usawiri wa Mwanamke katika Ngano 15

2.6 Pengo la Utafiti 16

2.7 Nadharia ya Utafiti 17

2.8 Hitimisho 22

SURA YA TATU 23

3.0 MBINU ZA UTAFITI 23

3.1 Utangulizi 23

3.2 Eneo la Utafiti 23

3.3 Usanifu wa Utafiti 23

3.4 Kundi Lengwa 24

3.5 Aina ya Utafiti 24

3.5.1 Maktabani 24

3.5.2 Uwandani 25

3.6 Sampuli na Usampulishaji 25

3.7 Vyanzo vya Data 26

3.7.1 Data za Upili 27

3.8 Mbinu za Kukusanya Data 27

3.8.1 Usaili 27

3.8.2 Upitiaji Nyaraka 28

3.9 Uchambuzi wa Data 28

3.9.1 Mkabala wa Kimaelezo 28

3.10 Hitimisho 29

SURA NNE 30

4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI WA DATA NA MATOKEO YA UTAFITI 30

4.1 Utangulizi 30

4.2 Jamii ya Wanyamwezi 30

4.2.1 Asili ya Wanyamwezi 30

4.2.2 Mahali Kijiografia 30

4.2.3 Utawala wa Wanyamwezi 31

4.2.4 Baadhi ya Mila na Desturi za Wanyamwezi 31

4.3 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data 32

4.3.1 Usawiri wa Mwanamke katika Ngano za Wanyamwezi 32

4.3.2 Ngano za Wanyamwezi na Namna Zinavyomsawiri Mwanamke 33

4.4 Hitimisho 46

SURA YA TANO 47

5.0 MUHTSARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 47

5.1 Utangulizi 47

5.2 Muhtasari wa Tasnifu 47

5.2.1 Usawiri wa Mwanamke katika Ngano Teule 48

5.2.2 Uhalisia wa Usawiri wa Mwanamke katika Ngano Teule 49

5.3 Utoshelevu wa Nadharia 49

5.4 Mapendekezo 49

5.4.1 Mapendekezo kwa Tafiti za Baadaye 50

5.5 Hitimisho 50

MAREJELEO 51

VIAMBATANISHO..... 54

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Tamko la Utafiti

Ngano ni utanzu wa fasihi simulizi ambao una historia ndefu katika kuwepo kwake hapa duniani. Ngano zimekuwepo tangu pale binadamu alipoanza kuwasiliana na wenzake kwa kutumia lugha (Mulokozi, 1996). Ngano zimekuwa ni chombo cha kutoa elimu kwa jamii katika maeneo mbali ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa kwa miaka mingi kabla ya ujio wa elimu ya kigeni iliyoletwa na wakoloni (Okpewho, 1992). Senkoro (1997) anaeleza kuwa mtu akitaka kuzifahamu mila na desturi za jamii fulani basi asome au asikilize ngano za jamii hiyo. Hii ina maana kuwa katika ngano kumehifadhiwa historia ya jamii pamoja na mambo mengine muhimu yanayoitambulisha jamii hiyo. Mawazo ya wataalamu hawa yanatufahamisha kuwa kuna aina mbalimbali za ngano ikiwa ni pamoja na hekaya inayojumuisha tarihi, ngano za mashujaa na ngano za mapenzi, Visasili na ngano zinazohusu wanyama (Okpewho, 1992).

Vipera hivi vya ngano vimekuwa vikitumika hata leo katika ulimwengu wa maandishi ambapo katika fasihi andishi tunawaona waandishi kama akina Shaaban Robert wakiandika riwaya ya Adili na Nduguze ambayo kimsingi ni sawa kabisa na hadithi ya hekaya. Hii ina maana kuwa riwaya hii imeandikwa kutokana na kisa cha masimulizi ya hekaya ambayo yalikuwa yakisimuliwa katika jamii kwa kipindi kirefu wakati wa kipindi cha masimulizi. Hadithi zinazohusu wanyama pia nazo bado zinaendelea kuandikwa na kutumika katika jamii. Baadhi ya watunzi wa kazi za

fasihi andishi ya Kiswahili wamekuwa wakiwatumia wahusika wanyama katika utunzi wa kazi zao ambazo ni fasihi andishi. Mulokozi anasema kuwa, ngano ni hadithi za kimapokeo zinazotumia wahusika kama vile wanyama, mazimwi na watu kueleza au kuonya kuhusu maisha. Kumbe wahusika wanyama ni wahusika wa kifasihi simulizi lakini siku hizi wahusika hawa hutumika katika ulimwengu wa fasihi andishi. Wahusika hawa hupewa matendo ya kibinadamu na hivyo kutoa funzo fulani kuhusu maisha kwa wanadamu.

Jamii zote za Kiafrika na duniani kote wanazo ngano ambazo huelezea hadithi mbalimbali kuhusu maisha. Okpewho (1992) anaeleza kuwa katika nchi ya Nigeria kwa mfano, kuna ngano za aina mbalimbali zinazohusu historia, asili ya watu na vitu, majanga kama misiba, zenye lengo la kuburudisha, kuonya na kuelimisha. Wamitila (2003) naye anaeleza kuwa katika nchi ya Kenya zipo ngano zenye mkondo kama huo na nyingi tayari zimeshaandikwa katika vitabu kwa lengo la kuzihifadhi. Nchini Tanzania pia kuna jamii zaidi ya 121 za makabila ambazo pia zinayo fasihi yake ikiwemo ngano. Kila kabila lina ngano zake ambazo huelezea masuala ya kihistoria, kijamii, kiutamaduni na kisiasa. Wanyamwezi ni miongoni wa kabila maarufu linalopatikana katika mkoa wa Tabora Magharibi mwa Tanzania. Jamii ya Wanyamwezi wamejaaliwa kuwa na ngano za hekaya, visasili, ngano za wanyama, tarihi, vigano na sira lakini hakuna watafiti ambao wamewahi kufanya utafiti wa kuzichunguza ngano hizo.

Utafiti kuhusu fasihi ya Wanyamwezi ni ule ambao ulifanywa na Richard (2002) aliyetafiti fani na maudhui katika methali za Wanyamwezi. Pamoja na mambo

mengine alibainisha kuwa muundo wa methali za Kinyamwezi unafanana sana na muundo wa methali za Kiswahili. Kwa kuwa methali za Kinyamwezi na za Kiswahili zote ni za Kibantu ni sharti muundo wake ufanane na hilo si jambo la mjadala. Hata hivyo, utafiti ni tofauti na wakwetu kwani huo ulihusu methali na huu wetu unahusu usawiri wa mwanamke katika ngano za Wanyamwezi.

Naye Mwamanda (2001) alitafiti nyimbo za Kinyamwezi kwa kuchambua vipengele vya dhamira na lugha ya falsafa inayojitokeza katika nyimbo za Kinyamwezi. Matokeo ya utafiti wake yanabainisha kuwa, nyimbo za Kinyamwezi zinamsawiri mwanamke kama mtu duni anayetegemea zaidi maamuzi ya mwanamume. Mwanamke ni mtu anayesawiriwa kuwa hawezi kuwa na mawazo mazuri na bora kuliko yale ya mwanaume na hivyo hawezi kushirikishwa katika maamuzi. Wanaume peke yao ndio walikuwa wakifanya maamuzi mbalimbali juu ya mustakabali wa jamii yao na wanawake wakiwemo ndani yake.

Kwa hakika hakuna watafiti watangulizi ambao wamechunguza namna mwanamke anavyosawiriwa katika ngano za jamii ya Wanyamwezi wa wanaopatikana mkoani Tabora. Utafiti huu umefanywa kwa lengo la kuziba pengo la maarifa kwa kubainisha namna mwanamke anavyosawiriwa katika ngano hizo.

1.2 Tatizo la Utafiti

Usawiri wa mwanamke katika kazi za fasihi ni dhamira iliyowavutia watafiti wengi wa fasihi ya ulimwenguni na lengo lao likiwa ni kutaka kufahamu namna mwanamke anavyosawiriwa katika kazi husika. Matokeo ya tafiti mbalimbali duniani yanaonyesha kuwa mwanamke anasawiriwa katika hali duni na hasi ikilinganishwa

na mwanaume (Kipkorir, 2004) na Kitundu (2012). Kwa kiasi kikubwa mwanamke anasawiriwa kama kiumbe ambaye ni malaya, mwenye wivu, mfitinishaji, mbeya, muovu na muongo. Pia, zipo kazi nyingine za fasihi ambazo zinamsawiri mwanamke kuwa ni mtu mchapakazi, mwenye msimamo, mama mlezi, kiongozi katika jamii na mwenye hekima na busara. Wakati haya yote yakifahamika katika kazi za fasihi kwa jumla bado hatujafahamu namna ngano za Wanyamwezi zinavyomsawiri mwanamke.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu moja na malengo mahususi mawili kama ifuatavyo:

1.3.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza taswira ya mwanamke katika ngano za jamii ya Wanyamwezi.

i) Kuchambua taswira ya mwanamke katika ngano za jamii ya Wanyamwezi.

ii) Kubainisha uhalisia wa taswira ya mwanamke katika ngano za jamii ya Wanyamwezi kwa jamii ya leo.

1.4 Maswali ya Utafiti

iii) Ni ipi taswira ya mwanamke katika ngano za jamii ya Wanyamwezi?

iv) Taswira ya mwanamke katika ngano za Wanyamwezi ina uhalisia gani kwa jamii ya leo?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu kitaaluma, kijamii, kinadharia na kisera. Kwa

upande wa kitaaluma utafiti huu utaonyesha bayana namna mwanamke anavyosawiriwa katika kazi za fasihi hususani katika ngano za jamii ya Wanyamwezi. Baadhi ya ngano zinahusu wanyama lakini wanyama hao wanawakilisha wanadamu wenye sifa za tabia za kimfumo dume na hivyo utafiti huu utawezesha kubainisha namna wanyama walivyo na uwezo wa kuwasawiri wanawake na wanaume ambao ndio huwabeza na kuwakandamiza wanawake. Pia, utafiti huu utakuwa ni rejeleo muhimu kwa watafiti wajao. Watafiti hao wanaweza kuwa walimu, wanafunzi na watu wengine ambao wanapenda kutafiti taaluma za lugha.

Kwa upande wa kijamii, utafiti huu utabainisha namna mwanamke anavyosawiriwa katika ngano za jamii ya Wanyamwezi na sababu ambazo zinafanya mwanamke asawiriwe hivyo anavyosawiriwa katika nyimbo hizo. Hii itasaidia kuifanya jamii ifunguke kifikra na kimtazamo katika kumuona mwanamke na kumpatia hadhi anayostahiki badala ya kumbeza na kumkandamiza.

Kwa upande wa nadharia, utafiti huu utakuwa ni ithibati tosha ya kuthibitisha nadharia ya Ufeministi kuwa ni nadharia imara katika kuelezea na kuchambua masuala ya yanayohusu nafasi ya mwanamke katika jamii. Nadhari hii ilikuja kutokana na jitihada na kutaka nafasi sawa baina ya mwanamke na mwanaume katika masuala yote ya maisha ya binadamu. Matokeo ya utafiti huu yanaweza kuonyesha mafanikio ambayo yameshafikwa mpaka hivi sasa.

Kwa upande wa sera, utafiti huu utatoa muongozo kwa watunga sera kuweza kuona mambo ambayo wanaweza kuyazingatia katika sera zao na yale ambayo

watayawekea msisitizo zaidi. Hii itasaidia kutungwa kwa sera ambazo zitaisaidia jamii kutatua changamoto mbalimbali za masuala ya kijinsia.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umehusisha ngano 10 (kumi) tu za Wanyamwezi zilichambuliwa ili kubainisha jinsi mwanamke anavyosawiriwa katika ngano hizo. Uteuzi wa ngano hizo kumi umetokana na muda, vifaa na fedha atakazokuwa nazo mtafiti kwa ajili ya utafiti huo. Ni maeneo manne tu Isikizya, Ilalwansimba na Igoko ndiyo yaliyoteuliwa kama vyanzo vya data. Ngano hizo zitahusu maisha ya ndoa, harusi na uchumi.

1.7 Mpangilio wa Tasinifu

Tasinifu hii ina jumla ya sura tano ambapo sura ya kwanza inahusu utangulizi ambapo vipengele kama usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa utafiti vimeelezwa. Sura ya pili imewasilisha mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia huku sura ya tatu ikiwasilisha mbinu za utafiti. Sura ya nne imewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti na sura ya tano imetoa hitimisho, muhtasari na mapendekezo.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii ni mapitio ya machapisho mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu. Maandiko na machapisho haya ni pamoja na vitabu, tasnifu na makala mbalimbali katika kuyapitia na kuyachambua maandiko haya mtafiti atayagawanya katika sehemu zifuatazo. Maandiko yatakayohusu tafiti mbalimbali juu ya ngano kama utanzu wa fasihi simulizi, maandiko yatakayohusu usawiri na nafasi ya mwanamke katika ngano za Wanyamwezi. Nia ya kufanya hivi ni kubainisha kile kilichokwisha fanywa na kuandikwa kuhusu mada ya utafiti ili kuweza kubaini pengo la utafiti.

2.2 Fasili ya Fasihi Simulizi

Wanjali (2011) anafafanua kuwa fasihi simulizi ni sanaa ambayo nyenzo kuu ya utunzi, uwasilishaji na usambazaji wake ni sauti pamoja na vitendo.

Finnegan (1976:1) anasema ni fasihi inayotegemea mtendaji anayeteua maneno kulingana na tukio husika. Mulokozi (1996:24) hayuko mbali na Finnegan (keshatajwa), anasema, fasihi simulizi ni fasihi iliyotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo na vitendo, anaendelea kuwa fasihi simulizi ni tukio linalofungamana na muktadha (mazingira) fulani ya jamii. Senkoro anaiona fasihi simulizi kuwa hubadilika kulingana na wakati.

Okpewho (1992) anatumia neno “oral literature” ambalo hutumiwa zaidi kurejelea fasihi simulizi. Anasema, fasihi simulizi ni fasihi inayotolewa kwa njia ya mdomo,

anasisitiza kuwa fasihi simulizi ni fasihi ya zamani inayosimuliwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kutokana na mawazo ya Okpewho msisitizo unaonekana kwamba fasihi simulizi ya Kiafrika ni ya zamani na kwa kuwa husimuliwa kwa mdomo haina budi kubadilika kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mawazo haya yanaungwa mkono na Kirumbi (1975) na Wamitila (2003) na Wanjala (2011). Wataalam wote hapo juu wanakubaliana kuwa fasihi simulizi ni kazi ya fasihi ambayo inawasilishwa kwa masimulizi ya mdomo kutoka kizazi kimoja kwenda kingine. Hali hii inatupatia sifa kadhaa za fasihi simulizi kama zinavyotajwa hapa chini:

i) Fasihi simulizi hutungwa hapo kwa hapo.
ii) Fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo.
iii) Fasihi simulizi hupokea mabadiliko kulingana na muktadha.
iv) Fasihi simulizi inategemea utendaji.
v) Fasihi simulizi hutegemea akili ya msimulizi.
vi) Fanani na hadhira huonana ana kwa ana.

Sifa hizi za fasihi simulizi zilituwezesha kuzielewa vizuri ngano za Wanyamwezi kwa sababu nazo pia ni sehemu ya fasihi simulizi na zimepambwa kwa sifa hizi. Hii ilitupatia fursa ya kuchunguza namna mwanamke anavyosawiriwa katika ngano za Wanyamwezi.

2.3 Ngano Kama Utanzu wa Fasihi Simulizi

Ngano kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali wa fasihi simulizi ni utanzu mmojawapo wa fasihi simulizi. Okpewho (1992) anaongelea uainishaji wa ngano za

Kiafrika na namna ya usimulizi wa ngazo za Kiafrika. Anaeleza kuwa kuna njia nne mpaka sasa ambazo zimetumiwa kuainisha ngano. Njia hizo ni unguli ambapo katika kigezo hiki zinajitokeza ngano zihusuzo wanadamu, ngano za wanyama, ngano za vichimbakazi na ngano za miungu. Anaeleza kuwa kigezo hiki kinaonesha kuwa na matatizo. Matatizo haya ni pamoja na kufanana kitabia kati ya jamii moja na nyingine. Kwa mfano, katika ngano za wanyama, wanyama hupewa uwezo wa kuzungumza, kufikiri, na kutenda kama wanadamu.

Kigezo kingine ni lengo la ngano husika, katika kigezo hiki ngano zinaainishwa kwa kuzingatia lengo la simulizi husika. Hapa panajitokeza ngano zinaainishwa kwa kuzingatia lengo la simulizi husika. Hapa panajitokeza ngano za kimaadili, ngano za kuhimiza kazi na ngano za kubembeleza mtoto. Ngano nyingi zilizopo katika kigezo hiki ni zile ambazo zinazungumzia maadili.

Kigezo kingine ni sifa ya ubora wa ngano ambapo kigezo hiki kinaonekana kubeba kundi kubwa la ngano. Katika kigezo hiki kuna ngano ayari – hizi huambatana na uelevu au ulaghai wa wahusika; ngano za matambiko na ngano za kihistoria ambazo huhusu vita, vizazi, mashujaa, usuli wa kitu au jambo fulani.

Kigezo cha nne ni muktadha wa utendaji wa ngano husika. Katika kigezo hiki kinachoangalia ni ngano inatendwa wakati gani na katika mazingira gani. Kwa mfano, kwa kutumia kigezo hiki tunaweza kupata ngano zinazotendwa wakati wa mbalamwezi ngano zinazotendwa wakati wa Ibada, ngano zinazotendwa wakati wa mapumziko ya wawindaji na nyinginezo.

Okpewho (ameshatajwa) pia anajadili usimulizi wa hadithi katika Afrika. Anaeleza kuwa msimulizi wa kijadi ni tofauti na yule anayepatikana katika maandishi. Pia Okpewho anaeleza kuwa, usimulizi katika Afrika unafanyika wakati maalum hasa wakati wa jioni au usiku watu wanapokuwa katika mapumziko baada ya vipindi maalumu vya kazi. Okpewho anaeleza kuwa usimulizi wa hadithi katika Afrika hufuata fomula maalum. Usimulizi wa hadithi hizi huwa na mianzo na miisho ya kifomula ingawa mianzo na miisho hiyo kutofautiana toka jamii moja hadi nyingine. Pia usimulizi wa hadithi unaambatana na ushiriki wa hadhira ambaye huonesha kuwa anafuatilia simulizi hiyo. Mtafiti ametumia mtazamo wa Okpewho kwa kuangalia ngano za Kinyamwezi za kimaadili ili kuona taswira ya mwanamke ikoje katika jamii ya kinyamwezi.

Msokile (1992) anasema, ngano ni hadithi ambazo hazina mshikamano kama zile hadithi za kisasa za Kiswahili bali zinaonekana kama kitu kimoja. Fasihi hii haina mashiko katika utafiti huu kwani haijafafanua maana ya ngano bali imelinganisha ngano na hadithi fupi za Kiswahili bila kueleza hadithi fupi za Kiswahili ni nini.

Mulokozi (1996) anasema ngano ni hadithi za kimapokeo zinazotumia wahusika kama wanyama, mazimwi na watu kueleza au kuonya kuhusu maisha. Fasili hii itamsaidia mtafiti katika mambo mawili ambayo, kwanza kabisa inasisitiza kuwa ngano hupokelewa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, hivyo basi katika uchambuzi wa data, Mtafiti alizingatia pia maisha ya sasa ya jamii ya Wanyamwezi kwa sababu ngano hubadilika kulingana na wakati ili kusawiri maisha ya jamii husika.

Naye Wamitila (2003) anasema kuwa, ngano ni hadithi za kale, ni mojawapo ya tanzu aa fasihi simulizi ambayo hupokezwana toka kizazi kimoja hadi kizazi kingine lakini hubadilika kutokana na ufaraguzi wa wasimulizi. Ngano zinaanza na fomula ya hapo za zamani za kale na wahusika wake ni wanyama na binadamu. Maelezo ya Wamitila yanaungwa mkono na King'ei na Kisovi (2005). Wanasema kuwa, ngano ni hadithi fupi na masimulizi yasiyo ya kishairi, katika hadithi hizi kuna wahusika ambao wanazungumziwa. Fasili hii haina mashiko katika utafiti huu kwani haijafafanua maana ya ngano kwani haijaeleza masimulizi ya kishairi ni yapi, pia haijafafanua wahusika wa ngano ni wapi bali imetaja tu kuwa kuna wahusika katika ngano.

Mwanazuoni mwingine ambaye ameongelea kuhusu ngano ni Senkoro (2011) anasema kwamba, ngano ni utanzu wa fasihi simulizi ambao hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo na wahusika wake ni wanyama, wadudu, mimea au mashetani. Amesisitiza pia lengo kuu la ngano ni kuielekeza jamii, kuonya, kuadibu, kufunza na kujenga utu bora. Hivyo basi, kutokana na fasili ya Mulokozi, Wamitila na Senkoro (wameshatajwa) twaweza kusema kuwa, ngano ni hadithi fupi za kubuni ambazo hurithishwa kutoka kuzazi kimoja hadi kingine kwa lengo la kuelimisha jamii fulani kuhusu maisha yao ya kila siku.

Maelezo kuhusu ngano yaliyotolewa na wataalamu hapo juu yanatufahamisha kuwa ngano huweza kuwa na sifa zifuatazo:

i) Ngazo zina mianzo ya kifomula kama vile hapo zamani za kale, hadithi hadithi.

ii) Wahusika katika ngano ni watu, wadudu, wanyama mizimu n.k.

iii) Ngano huwasilishwa kwa njia ya mdomo.

iv) Ngano zina mafunzo katika jamii husika.

v) Ngano kubadilika kutokana na kizazi kimoja hadi kingine.

vi) Ngano ni hadithi fupi.

vii) Ndani ya ngano kuna nyimbo, methali na misemo ambayo hubeba maudhui fulani.

viii) Ngano kubadilika kulingana na namna ya usimulizi, pia hadhira na jamii fulani.

Kutokana na mapitio hapo juu tunaweza kuona sifa za ngano ambazo zimebainishwa, hivyo basi hatuna budi kusema kuwa ngano ni utanzu wa fasihi simulizi kutokana na kuwa na sifa za fasihi simulizi.

2.4 Usawiri wa Mwanamke katika Fasihi Simulizi kwa Ujumla

Fasihi simulizi kwa ujumla katika kipengele hiki tutaangazia mapitio mbalimbali yatakayohusiana na usawiri wa mwanamke katika Fasihi Simulizi isipokuwa katika ngano. Lengo la kupitia mapitio haya ni kuona namna mwanamke alivyochorwa katika kazi hizo ili kuweza kupata picha kabla ya kuangazia utanzu wa ngano. Kazi yoyote ya fasihi haina budi kuwa na wahusika kwani ni kiungo muhimu ambacho kubebeshwa maudhui fulani ili kufunza jamii husika.

Mwanamke ni mmoja wapo wa wahusika katika fasihi ambaye hukusudiwa awakilishe dhana, mawazo au tabia za watu katika jamii. Miongoni mwa watafiti walifanya utafiti juu ya mhusika wa kike katika Fasihi Simulizi ni hawa wafuatao:

Balisidya (1982) alitafiti kuhusu taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi ya Kitanzania ambapo alijikita zaidi katika hadithi fupi, nyimbo na vitendawili na kuhitimisha kuwa mwanamke huchorwa kama mlezi wa familia, chombo cha starehe kwa mwanaume. Anaendelea kueleza kuwa mwanamke katika jamii ya Watanzania anatazamwa kama chombo cha starehe kwa mwanaume kitu ambacho yeye anakiona kuwa hakimpi heshima mwanamke kama mzazi bali chombo cha mwanaume kutimiza haja zake. Utafiti wetu umefanywa kwa lengo la kubainisha namna mwanamke alivyosawiriwa katika ngano za jamii ya Wanyamwezi na hatimaye kubainisha hadhi yake.

Chiraka (2002) alitafiti kuhusu nafasi ya mwanamke katika nyimbo za harusi za kabila la Wajita na kuhitimisha kuwa katika nyimbo hizo mwanamke ndiye anayeonekana kupewa mawaidha na maonyo peke yake. Maswali yanaibuka kutokana na hitimisho la Chiraka ni haya; Je ni yupi atakayetakiwa kuwa na maadili mema katika jamii? Kwa nini mawaidha na maonyo yamlenge mwanamke peke yake? Maswali haya kwa uwili wake yanatokana na kumwonya mwanamke peke yake wakati harusi ni ya watu wawili.

Kipkorir (2004) amechunguza nafasi ya mwanamke katika methali za Wakurya na kugundua kuwa methali za Wakurya zinamsawiri mwanamke katika pande mbili, upande wa kwanza ni ule unaompa hadhi mwanamke kama mlezi wa familia, mwenye heshima, mkombozi kwa kutaja baadhi. Upande wa pili ni ule unaomshusha hadhi mwanamke kama chombo cha starehe, mtumwa kwa mumewe, asiye na nafasi katika tendo la ndoa.

Kipkorir akimnukuu Tabisson (1996) anasema kuwa, wanawake wa Kikurya hawaruhusiwi kusimama mbele ya mkutano (kikaoni) wa wanaume, labda tu anakesi ya kujibu. Tobiisson anazidi kusisitiza matokeo ya utafiti wa Kipkorir kuwa katika jamii ya Abakurya mwanamke bado anapewa hadhi ya chini ukilinganisha na hadhi anayopewa na mwanaume. Hitimisho hili litatusaidia pia kuchunguza usawiri wa mwanamke katika ngano za Kinyamwezi ili kufahamu namna gani mwanamke anasawiriwa katika ngano za Wanyamwezi. Naye Mnenuka (2010/2011) katika makala yake amechunguza taswira ya mwanamke katika nyimbo za muziku wa kizazi kipya na kugundua kuwa mwanamke anachorwa katika mtazamo hasi. Mathalani katika nyimbo za offside Trick ambazo ni; ″Ndege? ″Samaki″ na ″Bata″.

Taswira hizi ni tofauti lakini zote kwa pamoja zinamsawiri mwanamke kama mwenye tabia mbaya, malaya aliyeshindikana, asiyeweza kutulia na mume mmoja, Mnenuka (2010/2011: 86-87) anahimiza namna taswira ya mwanamke inayojitokeza kulingana na dhana iliyokusudiwa. Anasema kuwa taswira zote hizo huonesha uhasi wa matendo na tabia za mwanamke, jambo litendalwo na mwanaume huwa chanya na litendalwo na mwanamke huwa hasi. Mitazamo ya watafiti hao itamchorea mtafiti kufanya utafiti ili kutambua namna mbali mbali ambavyo mwanamke atasawiriwa katika ngano za Kinyamwezi.

Ramadhani (2013) ametafiti usawiri wa mwanamke taarabu ya mipasho kwa kuchambua baadhi ya nyimbo za Mzee Yussuf. Katika uchambuzi wake Ramadhani amebainisha kuwa mwanamke bado anasawiriwa kama mtu aliye chini ya

mwanaume. Mathalani mtafiti atasema karibu kila wimbo kati ya zile tisa alizotafiti zinamsawiri mwanamke kama pambo na chombo cha starehe. Pitio hili litamsaidia mtafiti kutambua kuwa mbali na harakati za kumtetea mwanamke bado jamii itaendelea kumtazama kama chombo duni.

Mapitio ya kazi tangulizi hapo juu yanabainisha kuwa utafiti kuhusu nafasi ya mwanamke katika kazi za fasihi umefanywa kwa kiasi fulani ambacho bado hatuwezi kusema kuwa ni kikubwa. Sambamba na hilo, hatujaona utafiti ambao umeshughulikia taswira ya mwanamke katika ngano za jamii ya Wanyamwezi ndio maana tukaona kuwa kuna haja ya kufanya utafiti huu.

2.5 Usawiri wa Mwanamke katika Ngano

Kitundu (2012) alitafiti usawiri wa mhusika wa kike katika ngano za Kinyiramba mkoani Singida na kubaini kuwa mwanamke katika jamii yake bado amepewa nafasi duni ambayo inamdhalilisha mwanamke kama chombo cha starehe, malaya, bidhaa, mchawi na kiumbe dhaifu. Kitundu (2012) anahitimisha kuwa kinachorudisha nyuma maendeleo ya wanawake ni mfumo uliopo kati ya jamii ya taifa la Tanzania. Kuna mfumo ambao unamfanya mwanamke asiwe na nafasi sawa na mwanaume. Kazi hii ilimsaidia mtafiti katika kutambua mfumo wa jamii ya Kinyiramba Tanzania na kisha kuona kama unalingana na ule wa Kinyamwezi.

Naye Mbiu (2013) amechunguza usawiri wa mwanamke katika ngano za Kisambaa. Amegundua kuwa mwanamke amesawiriwa asiye na maamuzi, hana haki ya kumiliki mali, mzalishaji mkuu wa familia, ni jasiri, ni mtumwa kwa mwanaume.

Mtafiti anahitimisha kwamba mwanamke katika ngano za Kisambaa, mwanamke amesawiriwa katika mitazamo hasi na chanya lakini amesawiriwa zaidi katika mtazamo hasi. Mawazo ya pitio hili bado litampatia mchango mtafiti kuhusu usawiri wa mwanamke katika jamii ya Tanzania. Ingawa baadhi ya watafiti wamefanya utafiti kuhusu usawiri wa mwanamke katika ngano, utafiti katika jamii ya Wanyamwezi bado haujafanyika. Utafiti huu pia umeeleza sababu za mwanamke kusawiriwa kama alivyosawiriwa katika ngano za Wanyamwezi jambo ambalo tafiti zilizotangulia halijaligusia.

2.6 Pengo la Utafiti

Katika mapitio yaliyopitiwa katka Fasihi Simulizi kwa ujumla na katika ngano itabainika kuwa utafiti kuhusu usawiri wa mwanamke katika jamii ya Wanyamwezi bado haujafanyika. Pamoja na kuwepo kwa tafiti mbalimbali kuhusu ngano bado kuna pengo kubwa litakalojitokeza katika ngano za Wanyamwezi kwa sababu zifuatazo; Kwanza, jamii ya Wanyamwezi ina utamaduni wake tofauti na jamii nyingine, hivyo usawiri wa mwanamke katika ngano za Wanyamwezi utategemea kuwa tofauti na ule wa jamii nyingine. Pili, tafiti zilizotangulia hazijabainisha sababu za usawiri wa mwanamke katika ngano, zimeishia tu kueleza namna mwanamke anavyosawiriwa. Tatu, tafiti hizo hazijahusisha taswira ya mwanamke katika ngano na taswira za mwanamke halisi katika jamii. Hivyo, utafiti huu umekusudia kuziba pengo hilo kwa kueleza namna mwanamke anavyosawiriwa katika ngano za Wanyamwezi kisha kubainisha uhalisia uliopo kati ya taswira ya mwanamke katika ngano za Wanyamwezi na taswira za mwanamke katika jamii halisi ya Wanyamwezi.

2.7 Nadharia ya Utafiti

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya Ufeministi. Nadharia hii iliasisiwa kwa lengo la kuangalia na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii inayotawaliwa na wanaume. Matatizo yenyewe yanasababishwa na tofauti za kijinsia. Kwa maoni ya waasisi wa nadharia hii, matatizo yanayomkabili mwanamke yamejengeka kwenye misingi ya jinsia yao. Hii ina maana kuwa mwanamke amewekwa katika hadhi au daraja fulani katika jamii. Kulingana na Wamitila (2003:253), Ufeministi ni nadharia inayopinga asasi zote za kijamii zinazochangia katika kudhulumiwa kwa mwanamke. Wafuasi wa nadharia hii wanashikilia kwamba, pana haja ya kuwa na usawa wa kijinsia licha ya kuwapo kwa tofauti za kimaumbile. Kwa hivyo, wote wanaelekea kukubaliana kuwa, wanawake wanafaa wajitokeze kupigania haki zao ili angalau kuwe na usawa wa kijinsia.

Kulingana na Wafula na Njogu (2007:92), kuna njia mbili za kubainisha matapo tofauti ya nadharia ya Ufeministi. Kuna uainishaji unaoangazia masuala ya wanawake kimaeneo na uainishaji unaozingatia mirengo ya kiitikadi. Tumeangalia aina zote mbili. Uainishaji wa kimaeneo, kulingana Wafula na Njogu, ulifanywa kwa kuzingatia changamoto zinazowakabili wanawake katika maeneo mbalimbali. Uainishaji huu ulitokana na ufahamu kwamba, wanawake wanakabiliwa na matatizo na changamoto tofautitofauti kutegemea maeneo wanakotoka. Waligawa sehemu zenyewe katika makundi manne: Ufaransa, Marekani, Uingereza na Afrika.

Kulingana na wahakiki hawa wa kifeministi, wanawake wa Ufaransa walitilia mkazo matumizi ya lugha. Kwamba lugha ilitumiwa kwa kumpendelea mwanamume.

Wanawake wa Marekani waliwaunga mkono wale wa Ufaransa. Nao wakasema kuwa ni lugha na maandishi yaliyomtofautisha mwanamke na mwanamume. Wao walizingatia maandishi, namna mwanamke alivyojieleza na kukariri dhamira fulani katika maandishi yao. Wanawake wa Uingereza nao walitilia mkazo suala la siasa na historia. Kwa maoni ya wanawake hawa wa Uingereza, wenzao wa Marekani walisisitiza zaidi masuala ya kihisia na sanaa, na kusahau historia na siasa. Wanawake wa Afrika nao wakawa na mtazamo tofauti na wenzao wa Ulaya na wale wa Marekani. Kwao, suala la utamaduni ndilo liliwakabili. Suala hili lilikuwa linawanyima nafasi ya kujieleza kwa namna mbalimbali; kuwakosesha nafasi ya kujieleza, uwezo wa kuchagua kuwa mke au mzazi wa mwanajamii, tohara na ukeketaji pamoja na desturi zilizomdharau mwanamke asiyezaa. Kwetu, tutazingatia mwelekeo wa Kiafrika kwani tunaangazia masuala yanayowahusu wanawake wa bara la Afrika na hasa eneo la Afrika Mashariki. Uainishaji wa pili kama wanavyoangazia Wafula na Njogu, ulifanywa na Adamson, Briskin na McPhail. Wahakiki hawa walizingatia mirengo ya kiitikadi. Mirengo yenyewe ilizua mirengo mitatu ambayo ni; ufeministi huru, ufeministi wa kiharakati na ufeministi wa kijamaa. Ufeministi huru hutetea usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi zote za maisha. Mkondo wenyewe hushikilia kwamba, maadamu wanadamu wameumbwa kuwa viumbe sawa, wote wanawake kwa wanaume wanapaswa kuwa huru kutekeleza majukumu na malengo yao.

Ufeministi wa kiharakati humchukulia mwanamume kuwa adui mkubwa kabisa wa mwanamke. Waitifaki wake wanaamini kuwa uwezo wa mwanamke wa kuzaa ndio ambao hutumiwa na mwanamume kumdhalilisha. Kwa maoni yao, suluhu ni

kuwahimiza wanawake wasiolewe na wanaume. Badala yake wanawake wanahimizwa kushirikiana wao kwa wao hata kimapenzi. Ufeministi wa kijamaa nao hulenga kukosoa ujamaa wa kimapokeo ambao licha ya kudai kwamba msingi wa unyonyaji ni jamii ya kitabaka inayompa mwanamume uwezo wa kumiliki njia kuu za kuzalisha mali, kutumia mali hiyo kadiri ya uwezo wake, huendeleza utabaka katika misingi ya kijinsia. Mrengo huu unawahimiza wanaume kushiriki katika malezi ya watoto na kadhia nyingine ambazo kimapokeo zimechukuliwa kuwa kazi za mwanamke. Utafiti huu wetu utaegemea Ufemenisti wa eneo la Kiafrika. Huu ni Ufemenisti unaozingatia suala la utamaduni. Ufeministi wa Kiafrika hasa ule unaohusisha fasihi unajishughulisha na hali halisi katika jamii za Kiafrika. Nadharia yenyewe inaangazia jinsi miktadha tofautitofauti inavyochangia katika unyanyasaji, udunishaji na udhalilishaji wa mwanamke wa Kiafrika. Wataalamu wanaounga mkono nadharia hii wanaeleza hali kinzani. Kwao, badala ya wanawake kuyakabili matatizo yaliyomo, wengi wao wanayakwepa. Wanadhihirisha mielekeo ya kutaka kufurahisha na kutojali hali yenyewe. Hatua hii inamtia motisha mwanamume kumgandamiza mwanamke na kujihifadhia hadhi yake ya juu.

Mwasisi wa Ufeministi huu wa Kiafrika ni Filomena Steady (1981) anayefanua matarajio ya nadharia yenyewe. Kwake, nadharia inafaa kuchunguza hali za kijamii na kitamaduni zinazorutubisha unyanyasaji wa wanawake katika jamii. Nadharia yenyewe ina teneti zifuatazo: Inadhihirisha nia na malengo mahsusi yanayotokana na hali halisi katika jamii za Kiafrika. Inatambua historia ya jamii za Kiafrika, ambazo zilikuwa na watawala na mashujaa wanawake. Inachunguza hali ya mwanamke katika jamii ambazo zimekuwa na harakati za ukombozi na ujenzi wa jamii mpya.

Hivyo basi, nadharia hii ya Ufeminsti wa Kiafrika ni nadharia itakayotufaa zaidi. Itatufaa katika utafiti wetu wa kuchunguza nafasi na utambulisho wa mwanamke. Kwa maoni yetu, ni nadharia mwafaka inayotetea haki na usawa wa kijinsia katika jamii. Wafula na Njogu (2007:90) wanaelezea kuwa nadharia yenyewe inajumlisha mikabala mbalimbali ya kihakiki ambayo licha ya tofauti zake, inaelekea kukubaliana na kuafikiana kwenye masuala ya kimsingi. Kwanza, nadharia yenyewe imewekewa msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa wanawake kutokana na pingu za kitamaduni, kidini, kisiasa na kiuchumi. Kwa maoni yao hizi ni pingu ambazo zimejengeka kwenye msimamo na itikadi ya kiume. Kudhulumiwa kwa mwanamke kumerutubishwa na mfumo wa ki-ubabedume unaomwenzi mwanamume na kumtweza mwanamke.

Wollstonecraft (1792) ndiye anayetambuliwa kwa kuanzisha harakati za kumkomboa mwanamke kutokana na ‘pingu’ za kijamii zinazotokana na misingi ya ki-ubabedume na mpangilio wa kiume katika jamii. Katika kazi yenyewe, *A Vindication of the Rights of Women* (1792), mfeministi huyu aliupinga mfumo wa ki-babedume. Kwake mfumo wenyewe uliwapotosha vijana kiasi cha kuwafanya watambue ‘uwezo’ wa kiume katika jamii na kujitambulisha kwao au kulazimishiwa kuitikia desturi ya jamii yenyewe. Kama hatua ya kupiga vita mpangilio kama huo, Wollstonecraft alipendekeza elimu ya kibinafsi kwa nia ya kumtenganisha mtoto na ubabe-dume au wanafunzi wachanganywe madarasani na kupewa fursa ya kufurahia ujana wao na wakati huo huo wapewe shughuli za kutekeleza kwa ushirikiano. Anapinga vikali mazoea yaliyopelekea kutwezwa kwa mwanamke. Elimu ndicho chombo cha kupelekea usawa wa kijinsia na ukombozi wa mwanamke. Anafichua

hali ambapo mwanamke hutazamwa kama mwanamke ndipo baadaye aonekane kama binadamu. Anasema mtazamo huu ndio unaomdunisha na kumpa mwanamke hadhi ya chini baada ya mwanamume.

Kimsingi, Mapendekezo ya Mary Wollstonecraft ni kuundwa kwa jamii mpya yenye usawa kati ya mwanamke na mwanamume. Mawazo haya yanaungwa mkono na Simone de Beauvoir katika kazi yake ya *The Second Sex* (1949). Beauvoir anazishambulia asasi za kitamaduni zilizojengwa kwenye imani ya uwezo mkubwa alio nao mwanamume kiasi cha kumchukulia mwanamke kama kiumbe duni. Alikuwa na mawazo sawa na ya Wollstonecraft kwamba, jamii inaendeleza taswira fulani chukulizi kumhusu mwanamke. Inamwangalia mwanamke kama kitu hasi ilhali mwanamume ni binadamu kielelezo. Kwa mujibu wa Wamitila (2002:157), Beauvoir anasisitiza kuwa utamaduni anamokulia mwanamke huchangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge. Utamaduni huo hivyo basi, unamfanya na hata kumlazimisha mwanamke kukubali kuwa yeye ni kiumbe duni.

Hivyo basi, chimbuko la nadharia hii ni kupigania haki za usawa wa binadamu kusisitiza suala zima la ushiriki wa mwanamke katika masuala mbalimbali ya kijamii, sambamba na chimbuko la nadharia hii msingi wake mkuu hapo awali ulikuwa ni kueleza namna waandishi wanavyojihusisha na fasihi katika kumsawiri mwanamke. Wahakiki wa Kifeministi waligundua kwamba maendeleo yalitawaliwa na mfumo dume hivyo hata maudhui ya fasihi yalijikita kuelezea mfumo dume. Wahakiki pia walitambua kuwa kazi zilizotungwa na wanawake zilidharauliwa.

Baadaye Ufaministi ulianza kujihusisha na mambo yanayohusiana na mfumo dume katika jamii kama elimu, siasa na utendaji kazi.

Utafiti huu umetumia nadharia hii kwa sababu ni nadharia pekee inayozungumzia masuala ya wanawake kijamii, kisiasa na kiuchumi, katika uchambuzi wa ngano za Wanyamwezi ili kuweza kuchunguza namna mwanamke alivyosawiriwa, mtafiti ataangalia masuala ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni ambayo ni mazingira yatakayomzunguka mwanamke katika jamii. Uteuzi wa nadharia hii katika uchambuzi wa ngano za Wanyamwezi utazingatia unyanyasaji na ukandamizwaji wa mwanamke kijaamii, kisiasa na kiuchumi kama unavyoelezwa na Wanafeministi, utafiti wetu ulilenga kuchunguza namna mwanamke anavyosawiriwa katika ngano za Wanyamwezi. Hivyo basi, tumeitumia nadharia hii katika uhakiki wa ngano za Wanyamwezi katika kumsawiri mwanamke na kisha kuwezesha kujibu maswali ya utafiti wetu.

2.8 Hitimisho

Sura hii imepitia mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Mapitio ya kazi tangulizi yamebainisha kuwa hakuna utafiti wa kina ambao umeshafanyika kuhusu ngano za jamii ya Wanyamwezi na ndipo sisi tukaamua kufanya utafiti huu. Sura inayofuata inahusu mbinu za utafiti.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha na kuelezea mbinu mbalimbali za utafiti ambazo zimetumika katika kukusanya na kufanya uchambuzi wa data. Kothari (2008) anaeleza kwamba mbinu za utafiti ni muhimu katika utafiti wa kitaalumu kwa sababu ni kutokana na mbinu hizi ndipo utafiti unakuwa umefanyika kisanyansi. Mbinu za utafiti huu ni kama zifuatazo:

3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti umefanyika. Utafiti huu umefanyika katika mkoa wa Tabora. Ngano zilizotumika katika utafiti huu zilipatikana kutoka kwa wakazi wa Tabora hususani wazee na vijana ambao wanazifahamu vizuri ngano za Kinyamwezi. Utafiti ulifanyika katika wilaya ya Tabora vijijini (Uyui) tu, kwa sababu ni wilaya ambayo ina Wanyamwezi asilia ikilinganishwa na wilaya zingine zilizomo mkoani Tabora. Vijiji vilivyohusishwa katika ukusanyaji wa ngano ni vitatu ambavyo ni; Isikizya, Ilalwansimba na Igoko. Vijiji hivi vimeteuliwa kwa sababu kunapatikana Wanyamwezi nab ado wanasimuliana hadithi.

3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni ramani inayochorwa kuonesha sura nzima ya utafiti inavyopaswa kuwa tangu katika ukusanyaji wa data mpaka uandishi wa tasinifu nzima (Kothari, 2008; Babie, 1999). Kuna aina mbalimbali za usanifu wa utafiti, lakini katika utafiti huu tumetumia uchunguzi kifani. Uchunguzi kifani ni aina ya

usanifu ambao humpa mtafiti uhuru wa kuteua jambo moja mahususi ambalo atalichunguza kwa undani na kulitolea mahitimisho muafaka (Creswell, 2009). Good (1966) anaeleza kwamba, uchunguzi kifani ni mbinu nzuri ya utafiti kwa sababu ni ya uhakika inayomuwezesha mtafiti kupata taarifa muhimu na sahihi kwa kutumia muda na gharama ndogo ikilinganishwa na mbinu nyingine. Vile vile, uchunguzi kifani humuwezesha mtafiti kuuelewa muktadha mzima wa jambo analolitafiti na hivyo kuwa rahisi kwake kukamilisha malengo ya utafiti wake. Mbinu ya uchunguzi kifani inamsaidia mtafiti kujibu maswali kama vile nini? Kwa nini? Kwa sababu gani? Na kadhalika (Kothari, 2008). Utafiti wa kifasihi kama huu wetu hukusudia kujibu maswali ya aina hii. Kwa msingi huo basi, uchunguzi kifani umewezesha kukamilika kwa malengo ya utafiti wetu.

3.4 Kundi Lengwa

Walengwa wa utafiti huu ni wazee ambao wanazifahamu ngano za Kinyamwezi. Watafitiwa hawa wanafahamu vizuri ngano za Kinyamwezi na hivyo itakuwa rahisi kupata data za utafiti wetu. Mtafiti ameteua kundi hili hii kwa sababu ya urahisi wa upatikanaji wa data ghafi kuhusiana na mada ya utafiti, pia mkoa wa Tabora ni makazi ya mtafiti kwa sasa.

3.5 Aina ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa ni wa maktaba na uwandani kama inavyowasilishwa hapa chini:

3.5.1 Maktabani

Maktaba ni mahali maalum palipohifadhiwa nyaraka, vitabu, majarida, magazeti, yenye taarifa mbalimbali kwa masomaji na watafiti wa kada tofauti tofauti za

taaluma (Ewan na Lalver 2000). Maktaba zilizotumiwa katika utafiti huu ni za Maktaba ya Mkoa wa Tabora, Maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Katika maktaba hizi tulipitia na kusoma vitabu, makala, tasnifu, magazeti na tafiti tangulizi zinazoendana na mada ya utafiti wetu. Njia hii iliniwezesha kupata data za upili ambazo zimetumika kushadadia hoja za data za msingi.

3.5.2 Uwandani

Utafiti huu umekusanya data na taarifa mbalimbali zihusuzo mada ya utafiti kutoka uwandani. Berg (2007) anasema kwamba, uwandani ni mahali ambapo watu wanaishi na mtafiti anapokwenda kutafiti hupata data na taarifa ambazo ni mpya, halisi na ghafi ambazo hazikuwahi kukusanywa na mtu mwingine yeyote kwa minajili ya utafiti kama wake. Hivyo mtafiti alikusanya data kutoka katika vijiji vya Isikizya, Ilalwansimba na Igoko kwa sababu ndipo mahali ambapo Wanyamwezi wanaoendelea kughana ngano wanapopatikana.

3.6 Sampuli na Usampulishaji

Babbie (1999) anaeleza kwamba sampuli ni kundi dogo la watafiti wa linalochaguliwa katika kundi kubwa la populesheni kuu ambalo ndilo hutoa data za utafiti zinazowakilisha populesheni yote. Usampulishaji ni kitendo cha kuteua washiriki katika kundi kubwa la watafitiwa ili kupata idadi ndogo ya watafitiwa waliotumiwa katika kutoa data za utafiti. Naye Kothari (2004) anasema kuwa usampulishaji ni mchakato wa kupata taarifa kuhusu jamii nzima kwa kuchunguza sehemu tu ya jamii hiyo. Kutokana na fasili hizi tunaweza kusema kuwa sampuli ni

sehemu tu ya jamii ya watu fulani ambao huchaguliwa kuwakilisha jamii nzima. Aidha, utafiti huu umetumia sampuli lengwa katika kukusanya data za utafiti. Sampuli lengwa au wakati mwingine hufahamika kama sampuli madhumuni ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huteua watafitiwa wake akiwa anatambua kwamba watamsaidia kupata data anazozihitaji ili kujibu maswali yake ya utafiti. Sampuli lengwa ndio iliyotumika katika kupata usawiri wa wanawake katika ngano za Wanyamwezi kwasababu tunafahamu fika kwamba kutokana na sampuli hii tumepata data muafaka za kujibu maswali yetu ya utafiti.

Sampuli ya watafitiwa iliyotumika katika utafiti huu ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Kombo na Tromp (2006) wanafafanua usampulishaji lengwa kuwa ni mbinu ambayo mtafiti anavutiwa na uwakilishi wa dhana katika namna tofauti. Wanasisitiza kwamba mbinu hii hutumia zaidi kundi kubwa, kutokana na fasili hii tunasema kwamba sampuli hulenga kuchagua sampuli kwa makusudi kulingana na mahitaji ya utafiti.

Uteuzi wa sampuli umezingatia umri wa watafitiwa wa miaka 45-81 kwa sababu wana ufahamu mzuri wa ngano za Kinyamwezi. Sampuli hii iliundwa na watu 20 ambapo wanawake walikuwa 14 na wanaume 6 wenye umri kuanzia miaka 45-81 na walipatikana katika vijiji vya Isikizya, Ilalwansimba na Igoko. Hivyo, walengwa wa utafiti huu ni watu wa umri wa utu uzima na wazee kama miaka inavyoonekana.

3.7 Vyanzo vya Data

Utafiti huu umekusanya data za msingi na upili kama zinavyofafanuliwa hapa chini.

3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi ni halisi na hazijawahi kukusanywa na mtafiti yeyote Yule kwa madhumuni ya kujibu maswali ya utafiti yanayojibiwa katika utafiti huu. Ni data ghafi na ndio kwanza zinakusanywa kwa mara ya kwanza ili kujaza pengo la utafiti lililoachwa na watafiti tangulizi. Data hizi zilikusanywa kutoka katika simulizi za ngano kutoka jamii ya Wanyamwezi.

3.7.1 Data za Upili

Data hizi ni zile ambazo tayari zimekwisha kusanywa na watafiti wengine kwa minajili ya kujibu maswali ya utafiti wao. Data hizi zinapatikana katika vitabu, makala, majarida, tasinifu, tovuti na wavuti. Young (1984) anaieleza mbinu hii kuwa ni ya kukusanyia data mezani bila kuwafuata watafitiwa na kuwahoji ama kuwasaili kuhusiana na ukusanyaji wa data wa utafiti husika. Data hizi zilikusanywa katika machapisho mbalimbali ambayo yanahusiana na mada ya utafiti huu.

3.8 Mbinu za Kukusanya Data

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu zifuatazo:

3.8.1 Usaili

Kothari (2008) anaeleza kuwa usaili ni mbinu ambayo humpa mtafiti fursa ya kukutana ana kwa ana na watafitiwa wake na kufanya nao mahojiano juu ya mada ya utafiti wake. Mtafiti hutakiwa kuandaa maswali ambayo atayatumia kama muongozo wa mahojiano yake na watafitiwa. Kuna aina kuu mbili za usaili ambazo ni usaili funge na usaili huru. Usaili funge ni ule ambao unamwelekeza mtafiti kuandaa

maswali ambayo yanamwelekeza mtafitiwa kutoa jibu maalum linalotazamiwa kutoka katika machaguo machache tu. Aina ya pili ya usaili ni usaili huru ambapo maswali ya usaili hutoa uhuru kwa watafitiwa kujibu maswali kwa kutoa maelezo kadri wanavyolifahamu jambo waliloulizwa bila kikomo. Katika utafiti huu tumetumia aina zote mbili za usaili kwa lengo la kupata data tulizokuwa tunazihitaji. Tumefanya usaili na jumla ya watafitiwa 20 ambao walikuwa ni wazee 20 ikiwa ni wanaume 6 na wanawake 14. Usaili ni mbinu muafaka katika utafiti huu kwani watafitiwa 20 waliweza kusailiwa na kuwezesha kupata ngano za kutosha.

3.8.2 Upitiaji Nyaraka

Mosha (2004) anasema kwamba, upitiaji wa Nyaraka ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambazo taarifa zake hukusanywa kutoka katika maandiko mbalimbali yanayohusiana na utafiti husika. Data zinazohusiana na mada hii ya utafiti zilikusanywa katika maktaba mbalimbali Mkoani Tabora kama vile Maktaba ya Mkoa, Maktaba ya Chuo kikuu cha Teofilo Kisanji, Maktaba ya Chuo cha Ualimu Tabora na Maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora.

3.9 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data huaanza mara tu baada ya kukusanya data. Katika utafiti huu data zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo.

3.9.1 Mkabala wa Kimaelezo

Babbie (1999) anaeleza kuwa mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kuchambua data kwa mtafiti kutoa maelezo yenye kufafanua data zake za utafiti. Maelezo hayo ni

lazima yaendane na malengo mahususi ya utafiti ili mwishoni ionekane kuwa malengo hayo yamekamilika. Kwanza mtafiti alizitafsiri ngano toka lugha ya Kinyamwezi kwenda katika Kiswahili. Ngano zote zilizowasilishwa katika sura ya nne zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Data za utafiti huu zimewasilishwa kutoka na ngano moja baada ya nyingine na kisha ngano hiyo kuchambuliwa na kulingana na namna inavyomsawiri mwanamke.

3.10 Hitimisho

Sura hii imejadili mbinu na aina mbalimbali zilizotumika katika utafiti huu. Vipengele vilivyowasilishwa ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa, mbinu za kukusanya data na mbinu za kuchambua data. Sura inayofuata inashughulikia uwasilishaji, uchambuzi wa data na matokeo ya utafiti kulingana na malengo ya utafiti.

SURA NNE

4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI WA DATA NA MATOKEO YA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti. Data hizo zinajumuisha ngano pamoja na maoni ya watafitiwa. Mbinu ya mkabala wa kimaelezo ndiyo iliyotumika katika uchambuzi wa data kwa sababu utafiti huu ni wa maelezo zaidi.

4.2 Jamii ya Wanyamwezi

Katika sehemu hii tumeeleza historia fupi kuhusu jamii ya Wanyamwezi kama ifuatavyo:

4.2.1 Asili ya Wanyamwezi

Wanyamwezi ni jina walilopewa na watu wa pwani lenye maana ya watu kutoka upande wa magharibi. Kabila hili ni mkusanyiko wa makabila madogomadogo kama Wasumbwa, Wakonongo, Wakimbu, Wasagali na Wanyanyembe. Asili ya Wanyamwezi ni muunganiko wa makabila madogo madogo yaliyoungana chini ya utawala wa mtemi.

4.2.2 Mahali Kijiografia

Tabora ni mkoa ulio magharibi inapakana na mkoa wa kigoma na kusini inapakana na mkoa wa Shinyanga. Upande wa Maghribi inapakana na Mkoa wa Kigoma na Kusini inapakana na mikoa ya Rukwa na Mbeya. Wilaya za mkoa huu ni Tabora vijijini (Uyui), Urambo, Nzega, Igunga na Kaliua.

4.2.3 Utawala wa Wanyamwezi

Kabla ya kuja kwa wakoloni jamii ya Wanyamwezi ilikuwa chini ya utawala wa mtemi. Utemi ulikuwa ni utawala wa kurithishana kwa koo. Kulikuwa na koo maalum ambazo ndizo zilitawala tu. Kabeya (1966:5) anasema mtemi Nshimba alimpeleka mtoto wake Sibuga akatawale Ulyanhulu. Kabeya anaainisha watemi kumi na nane waliotawala Ulyanhulu nao ni Sibuga, Mkindo, Mlolwa, Moto, Nshimba Mchembe, Kapaya, Kasele, Kasimana, Mkindo II, Mirambo, Mpandashalo, Katuga, Kazwika, Kaswa, Kibete, Mirambo II, Sibuga II, Mkindo III. Hiyo basi Kabeya anathibisha kuwa utawala wa Wanyamwezi ulikuwa wa kurithishana kwa koo.

4.2.4 Baadhi ya Mila na Desturi za Wanyamwezi

Katika jamii ya Wanyamwezi baadhi ya mambo hutofautiana lakini mambo ya msingi hufanana miongoni mwa mambo hayo ni:

4.2.4.1 Dini

Wanyamwezi wanaamini dini ya Ukristo na uislamu pia, hapo awali kabla ya kuja kwa wakoloni waliamini zaidi miungu ambayo hadi sasa inaendelezwa kupitia matambiko kama kutoa sadaka za wanyama na sherehe.

4.2.4.2 Kuzaliwa na Ndoa

Wanyamwezi walikuwa na sherehe za kumkaribisha mtoto aliyezaliwa ingawa kwa sasa zinafifia kutokana na mwingiliano wa tamaduni. Katika suala la ndoa mtoto wa kiume ndiye anayechumbia, mtoto wa kiume huenda kwao na binti kuongea na

wazazi wa binti huyo kuhusu uchumba na ndoa Wazazi wa binti wakikubali ndipo mahari hupangwa na ikishatolewa ndipo ndoa hufungwa.

4.2.4.3 Maisha ya Familia

Familia nyingi huundwa na baba, mama na watoto lakini baba ndiye huwa na mamlaka katika nyumba.

4.3 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Jamii ya Wanyamwezi ina ngano ambazo zinasimuliwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Katika utafiti huu ngano zaidi ya kumi zilikusanywa lakini kutokana na malengo ya utafiti ngano kumi tu zilichambuliwa. Ngano hizi ni: mke wa Mwa Bhabha (Mama wa Kambo), Mfumu wa Nshimba (Mganga wa Simba), Mpulungu wa Mwipori (Mjanja wa Porini), Rhoda (Rhoda), Bhabha Mbhi (Baba Mbaya), Nzala ya Mchalo (Njaa Kijijini), Mkima Mgumba(Mwanamke Tasa), Msungwi (Msungwi) Mtemi Mbhi (Mfalume Mbaya), Mwana wa Mtemi. (Mtoto wa Mfalme). Ngano hizi zimewasilishwa na kuchambuliwa kwa mujibu wa kile kilichotakiwa katika malengo mahususi ya utafiti wetu.

4.3.1 Usawiri wa Mwanamke katika Ngano za Wanyamwezi

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi mawili ambayo yalikuwa ni kuchambua taswira ya mwanamke katika ngano za wanyamwezi na kisha kuelezea uhalisia wake kwa jamii halisi ya leo. Uwasilishaji na uchambuzi wa data ni kama ifuatavyo:

4.3.2 Ngano za Wanyamwezi na Namna Zinavyomsawiri Mwanamke

Ngano za jamii ya Kinyamwezi zinamsawiri mwanamke katika sura mbalimbali kama ifuatavyo:

4.3.2.1 Simulizi ya Mama wa Kambo

Hadithi! Hadithi!

Hadithi njoo!

Hapo mwanzo za kale palitokea baba mmoja aliyeitwa Tununonere. Tununonere alikua na wake wawili lakini Bi Mkubwa aliamua kuondoka na kwenda kwao na kuacha mtoto mmoja wa kiume. Bi Mdogo ambaye alibaki alikua na watoto wawili.

Siku moja Bi Mdogo alimwambia mwanawe akamkamate mtoto wa Bi Mkubwa atakapokwenda kuchunga. Wakati mtoto wa Bi Mdogo anamfukuza mtoto wa Bi Mkubwa ng'ombe walipotea. Kijana wa Bi Mkubwa alianza kuwatafuta. Alipokuwa akiwatafuta njiani alikutana na Bi Kizee. Bi Kizee alimwulizia 'unakwenda wapi mjukuu wangu'? Yule kijana alijibu 'nimepoteza ng'ombe wangu'. Bibi akamwambia 'nilambe kidonda changu, ukimaliza kukilamba kipige ngumi'. Mara alipokipiga kile kidonda cha bibi kakatokea kaumbwa kadogo. Bibi akamwambia kijana akafuate kambwa atawapata ng'ombe wake. Alipoanza kuondoka kambwa kakaanza kuhisi harufu ya ng'ombe hadi akawapata.

Alipowapata ng'ombe alikwenda nyumbani, alifika usiku sana na kuwafungia ng'ombe zizini. Asubuhi iliyofuata baba yake akamwambia akachunge ng'ombe tena, kijana aliondoka na kukaacha kambwa kake nyumbani. Alipoondoka Bi Mkubwa akaanza kuwaambia wanawe kuwa yeye hawezi kuishi na yule kijana hivyo ameamua kumwekea sumu kwenye ugali ila wasimwambie.

Yule kijana alipotoka kuchunga ng'ombe aliwafungia zizini. Kumbe yule mbwa alikuwa wa ajabu alimfuata Yule kijana na kumwambia kuwa ule ugali alioachiwa una sumu, hivyo asiule. Yule kijana hakula akalala. Hadithi ikaishia hapo.

Hadithi hii ilisimuliwa na Juma Rashidi kutoka katika kijiji cha Isikiziya tarehe 14.09.2013 saa kumi jioni. Ngano hii inapatikana katika muktadha wa nyumbani kwa sababu inasimulia maisha ya nyumbani maisha ya ndoa za mitala na namna mama wa kambo anavyoishi na mtoto wa mke mwenza.

Katika ngano hii mwanamke kasawiriwa kwa namna tofauti. Kwanza kabisa mwanamke anasawiriwa kama mtu asiye na maamuzi katika ndoa. Hii inadhihirishwa hali ya ndoa ya Tununonere ambaye alioa wanawake wawili. Katika ngano hii mwanamke anaonekana kutokuwa na maamuzi katika ndoa isipokuwa mwanaume ambaye ana maamuzi hata ya kuoa mke zaidi ya mmoja.

Pili, mwanamke anaonekana ni mtu mwenye uwezo wa kukomboka kifikra. Bi Mkubwa ambaye anatoroka baada ya kushindwa kuishi maisha ya ndoa za mitala ni mfano mzuri wa ukombozi wa kifikira. Tatu mwanamke anasawiriwa kama mtu mwenye huruma. Kutokana na huruma aliyokuwa nayo Bi Kizee anamsaidia mtoto aliyepoteza ng'ombe na kuweza kuwapata. Nne, mwanamke anasawiriwa kama mtu katili. Kitendo cha Bi Mdogo kuwaambia watoto wake wamkamate mtoto wa Bi Mkubwa na kupanga kumpa sumu kinamsawiri mwanamke kama mtu katili. Katika maisha halisi ya jamii ya leo wapo baadhi ya wanawake ambao hufanya ukatili dhidi ya watoto wa mke mwenzie. Jambo hili si zuri na halipaswi kuachwa likaendelea kwani ni hatari kwa mustakabali wa maendeleo ya taifa letu (Kitundu, 2012). Suala la mwanamke kuwa na huruma hilo halina shaka kwani hata katika ulimwengu wa leo wapo wanawake wengi wenye huruma na ndio maana huweza kuwalea watoto tangu wakiwa tumboni kisha kuwazaa na kuwalea mpaka pale wanapoweza kujitegemea wao wenyewe.

4.3.2.2 Simulizi ya Mganga wa Simba

Hapo zamani za kale palitokea wanyama walioishi pamoja. Siku moja Simba alisema wanyama wote wazee wakamatwe Sungura hakufurahia maneno ya Simba.

Alimficha bibi yake pangoni akawa anampelekea chakula na maji kila siku.

Siku moja Simba alikuwa amelala ameacha mdomo wazi. Nyoka alifikiri ule mdomo ni pango akaingia ndani. Simba aliamka akasikia tumbo lake zito sana akawaita waganga wote wakampa dawa lakini hakupona. Sungura alimweleza Simba kuwa bibi yake ni mganga mkuba sana, aliongeza kuwa bibi yake ni mzee naye anaogopa kukamatwa. Simba alifurahi akaahidi kuwa hatamkamata bali atampa zawadi.

Bibi yake Sungura aliitwa akakubali kumtibu Simba alikwenda porini akamshika panya akamleta mbele ya Simba. Akamwambia Simba apanue mdomo wake. Bibi yake Sungura alimfinya panya akalia. Nyoka aliposikia mlio wa panya akatoka tumboni mwa Simba. Bibi yake Sungura alimwachilia panya naye akakimbia. Nyoka alimfukuza panya. Simba akawa amepona kabisa. Baada ya kupona Simba alimpa bibi yake Sungura zawadi. Nimemaliza hadithi.

Hadithi hii ilisimuliwa na Hadija Haroun kutoka katika kijiji cha Ilalwansimba tarehe 21.09.2015 saa kumi jioni. Ngano hii inapatikana katika muktadha wa porini lakini inahusisha maisha ya porini na maisha ya nyumbani hivyo wahusika wanyama wamepewa uwezo wa kibinadamu ili kuakisi misha ya wanadamu.

Katika ngano hii Simba anaugua tumbo, anawaita waganga mbalimbali lakini wanashindwa kumtibu isipokuwa bibi yake sungura ambaye anaweza kumtibu kuwa nyoka aliingia tumboni mwa Simba. Hivyo basi, mwanamke amesawiriwa kama mtu

menye uwezo mkubwa wa kiakili na nguvu za ajabu za kuweza kutambua kwamba Simba alikua amemeza nyoka hivyo katika ngano hii mwanamke amekwezwa kiakili kuliko mwanaume. Katika maisha halisi zipo baadhi ya jamii ambazo zinafanya kazi ya kuua vikongwe kutokana na imani za kishirikina. Hili ni jambo baya ambalo linatakiwa kukomeshwa katika jamii.

4.3.2.3 Simulizi ya Mjanja wa Porini

Hadithi! Hadithi!

Hadithi njoo!

> Hapo zamani za kale palitokea wanyama wengi walioishi pamoja. Wanyama hao ni Sungura, Fisi, Nyati, Swala, Kobe, Nyani, Simba na wengine kama Twiga, Nyumbu na kadhalika.
> Siku moja Mfalme wao aliitisha kikao ili kutatua tatizo la maji lililowasumbua kwa muda mrefu. Mfalme wao alisimama na kufungua kikao wanaume! Kisha kuwakaribisha wanyama wengine wachangie mawazo yao. Mchangiaji wa kwanza alikuwa ni Simba alisimama na kusema ‘Ahsante Mfalme kunipa nafasi hii. Kwa mtazamo wangu napenda tuweke umoja na kuchimba kisima chetu hapa msituni’ wanyama wengine walipiga makofi na kumpongeza Simba kwa wazo zuri.
>
> Mchangiaji wa pili alikuwa ni Sungura alisema ’naunga mkono hoja ya mchangiaji aliyepita kwa asilimia zote. Swala naye alisema ‘mawazo waliyotoa wenzangu ni mazuri sana lakini nina changamoto. Simba na Sungura wana kucha za kuweza kuchimba ardhi na sisi tusiokuwa na kucha tufanyeje? Wote kwa pamoja walimjibu ‘tutatumia pembe zetu’. Wote walikubaliana na kupanga siku ya kuanza kazi.
>
> Siku ilipofika wote walikusanyika ili kuendelea na uchimbaji wa kisima isipokuwa Sungura pekee hakuonekana. Walichimba kisima na maji yakatoka masafi na mazuri lakini maji hayo yalianza kuchafuka. Mfalme aliitisha kikao tena ili wapeane zamu ya kulinda kisima ili kumpata mtu aliyekuwa akichaua kisima. Mlinzi wa kwanza alikuwa ni Simba ambaye aliamini angemkamata Sungura. Mara usiku wa manane Sungura aliingia kisimani na kibuyu cha asali na kumdanganya Simba kwa asali kisha kumfunga kwa kamba kwenye mti.

> Wanyama waliofuata pia hawakumkamata Sungura. Ilipofika zamu ya Kobe alikuwa na hasira na alidhamiria kumkamata. Alifanikiwa kumkamata na kuwasubiri wanyama wengine waje kwa mahojiano. Hadithi ikaishia hapo.

Hadithi hii ilisimuliwa na Neema Haji kutoka katika kijiji cha Igoko tarehe 07.09.2015 saa kumi jioni. Ngano hii inapatikana katika muktadha wa porini lakini inaakisi maisha ya binadamu kupitia wanyama. Ngano hii inasimulia ukosefu wa maji huko porini. Mfalme anaitisha kikao cha wanaume ili wajadili namna ya kuondokana na tatizo la maji. Katika kikao hicho wanaume pekee wanajadili kuchimba kisima na kukubaliana kuweka zamu ya ulinzi bila kuwashirikisha wanawake. Katika ngano hii mwanamke anasawiriwa kama mtu asiyeshiriki katika maamuzi ya kisiasa katika jamii kwa kuwa hajashirikishwa kabisa wala kutajwa. Katika ulimwengu halisia hili ni jambo la kawaida ambapo wanaume pekee ndiye huaminika kuwa wana ujuzi na maarifa ya kushiriki katika maamuzi huku wanawake wakiwekwa pembeni (Koda, 2000). Sababu kubwa ya hali hii ni mfumo dume ambao umetawala katika jamii wa kumuona mwanaume kuwa ni bora kuliko mwanamke.

4.3.2.4 Simulizi ya Rhoda

> Hapo zamani za kale palitokea baba mmoja na mama mmoja mabazo waliishi miaka mingi bila kupata mtoto. Mungu aliwajalia wakapata mtoto mmoja wakamwita Rhoda lakini yule baba hakuridhika na mtoto mmoja akaoa tena mke wa pili na kuzaa watoto wawili.
>
> Siku moja Bi mkubwa aliondoka na kwenda amsibani mara watoto wa Bi mdogo wakaenda kwao Rhoda. Wakamwambia Rhoda wakatafute kuni, Rhoda aliwakatalia na kusema kuwa ana kazi. Siku ya pili wakampitia tena akawaambia hawezi kwenda atakwenda siku iiyofuata. Siku ya tatu ilipofika wakampitia tena naye akakubali wakaenda kutafuta kuni. Walipofika porini wakaanza kukusanya kuni mara wakamwabia Rhoda afuate kuni

> mbali kidogo. Alipozifikia zile kuni akaona shimo. Akawaambia wenzake nao wakamsihi asiogope. Alipokuwa akichukua zile kuni mara akaingia ndani ya shimo na wenzake wakamfukia na kufunga kuni na kurudi nyumbani.
>
> Walipofika nyumbani mama Rhoda akawauliza ‘Mwanangu mmemwacha wapi? Walijibu kuwa Rhoda alisema anatangulia. Muda si mrefu bibi mmoja alikwenda porini kukusanya kuni. Alipokuwa anakusanya kuni alisikia sauti ya mtu ikiimba.
>
> *Ewe bibi mchanja kuni moja, mbili, tatu,*
> *Kamwambie baba na mama wamenifukia shimoni.*
>
> Yule bibi akashangaa kidogo lakini sauti iliendelea kuimba. Bibi alikwenda kwao Rhoda kuwapa taarifa. Walipofika baba Rhoda alianza kumfukua kwa huzuni huku mama Rhoda akiimba kwa huzuni.
>
> *Jamani! Jamani! Mtoto wangu unaniacha*
> *Unaniachia majonzi*

Hadithi hii ilisimuliwa na Bi. Agnes Shija kutoka katika kijiji cha Igoko tarehe 07.09.2015 saa kumi jioni. Ngano hii inapatikana katika muktadha wa nyumbani kwa sababu inasimulia maisha ya ndoa za mitala na mwanamke kama mlezi wa familia.

Katika ngano hii mwanamke anasawiriwa kama ifuatavyo: Kwanza kabisa mwanamke anasawiriwa kama mtu anayeolewa ili kuzaa watoto. Tunamwona baba Rhoda na mama Rhoda wanazaa mtoto mmoja, Baba Rhoda hakuridhika na mtoto mmoja ambaye ni Rhoda hivyo anaamua kuoa mke mwingine ili apate watoto wengi. Pili mwanamke anasawiriwa kama mtu katili. Watoto wa Bi Mkubwa wanapanga njama za kumwua Rhoda kwa kumtubukiza shimoni na kumfukia, hivyo kupitia wahusika hawa mwananmke anaonekana kama katili. Tatu mwanamke anaonekana kama mtu mwenye huruma, tunamwona Bi Kizee anakwenda kwao Rhoda kutoa

taarifa juu ya Rhoda kumtumbukizwa shimoni. Kitengo hiki ni cha huruma kwani asingekuwa na huruma asingeweza kufanya hivyo. Katika jamii ya leo wapo baadhi ya wanawake ambao wanateseka kutokana na kukosa watoto wakati mwingine ikiwa ni mume ndiye hana uwezo wa kumpa ujauzito. Lakini kutokana na mfumo dume mwanamke ndiye ambaye huhesabiwa kuwa hana kizazi ni mgumba na si mwanaume (Mlacha, 1996). Kitendo hiki si cha kiungwana na hakitakiwa kufumbiwa macho. Inapotokea tatizo kama hilo ni vizuri mke na mume wote wakaenda hospitali kutazamwa kwa vipimo maalum ili kubaini tatizo na kisha kulishughulikia.

4.3.2.5 Simulizi ya Baba Mbaya

> Palitoka baba mmoja na mama mmoja ambao waliishi vizuri. Wazazi hawa walizaa watoto watatu wakike. Siku moja mama na wanawe walikwenda msituni kukusanya kuni. Mara Simba akatokea na kuanza kuwafukuza na walipokuwa wanakimbia mtoto mmoja alikamatwa na Simba. Yule mama na wanawe wawili walirudi nyumbani.
>
> Walipofika nyumbani mumewe alimwuliza 'Mtoto wangu mwingine yuko wapi? Mkewe alimjibu 'Amekamatwa na Simba'. Basi yule baba akamfukuza mkewe na kubaki na wanae wawili. Baada ya mwaka mmoja Yule baba akaanza kuwatamani watoto wake akaanza kufanya nao mapenzi. Hao watoto hawakupenda tabia ya baba yao. Siku moja wakaamua kumsimulia jirani alikuwa ni Bi Kizee. Yule Bi kizee aliwashauri wamshitaki baba yao kwa wazee, walimshitaki na wazee wakampa adhabu ya kuhama kijiji kile kwani amekidharirisha kijiji na jamii nzima.

Hadithi hii ilisimuliwa na Bi. Zaituni Juma kutoka katika kijiji cha Ilalwansimba tarehe 14.09.2015 saa kumi jioni. Ngano hii inapatikana katika muktadha wa nyumbani kwa sababu inasimulia maisha ya familia ya baba watoto wake wawili wa kike.Katika ngano hii mwanamke anasawiriwa kama ifuatavyo: Kwanza kabisa mtu

asiyemiliki mali na watoto, katika ngano hii mwanamke anafukuzwa na mumewe baada ya mtoto wao kupotea. Pili mwanamke anawawiriwa kama mtu asiye na maamuzi juu ya mwili wake. Tunamwona baba anawaingilia kimwili watoto wake bila ridhaa yao, kitendo hiki kinaonesha mwanamke hana amri juu ya mwili wake. Tatu mwanamke anasawiriwa kama mshauri mzuri. Tunamwona Bi kizee anawapatia ushauri wasichana wawili kumshitaki baba yao ili ashitakiwe dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia na ushauri huu unafanikiwa na baba yao anachukuliwa hatua za kisheria.

4.3.2.6 Simulizi ya Njaa Kijiini

> Katika kijiji kimoja palitokea njaa kali sana mzee Milambo na familia yake pia hawakuwa na chakula. Kila siku mzee Milambo na wenzake walitoka kwenda kutafuta chakula. Mzee Milambo alikwua na tabia ya uchoyo. Kila alipoleta mihogo alimpatia mke wake asage kwenye jiwe. Mkewe alikuwa anasaga na kuhifadhi unga. Walikuwa wanakula kidogo na kuhifadhi unga mwingine. Lakini mke wa Milambo alikuwa anashangaa unga uliokuwa unabaki hawauoni. Alipomwuliza mumewe alichukia sana.
>
> Siku moja mkewe Milambo alisema hatalala usingizi wa fofofo, alitaka kumjua mwizi wa unga. Usiku ulipofika alimwona mumewe anaamka na kupika ugali na kule peke yake. Mkewe akaamka na kumwambia mumewe ‘Kumbe huwa unakula peke yako’? Mzee Milambo alichukia sana kwani siri yake imegunduliwa. Hivyo alimpiga mkewe na kumwua.

Hadithi hii ilisimuliwa na Bw. Robert Kaombwe kutoka katika kijiji cha Isikizya tarehe 21.09.2015 Saa kumi jioni. Ngano hii inapatikana katika muktadha wa nyumbani kwa sababu inasimulia maisha ya nyumbani na kijijini ambapo njaa kali inatokea na kuathiri maisha ya familia na kijiji.

Katika ngano hii mwanamke anasawiriwa kama ifuatavyo: Kwanza ni mlezi mwema kwa familia yake. Mama Milambo ni mwanamke anayeipenda familia yake ingawa

kuna ukosefu wa chakula kijijini lakini kinachopatikana anakula na watoto wake. pili mwanamke pia anasawiriwa kama mtu anayefanya kazi nyingi za nyumbani ili kuhakikisha kwamba familia yake inapata mahitaji muhimu. Mama Milambo anaonekana kusaga mihogo kwenye jiwe ili watoto wake wapate chakula. Katika maisha halisi ya jamii ya leo bado mwanamke ndiye mlezi mkuu wa watoto ikilinganishwa na wanaume. Hata katika mazingira ambayo mama anafanya kazi ofisini hutafuta msichana ambaye ndiye hubaki na watoto nyumbani. Huyu msichana ni mama na ndiye mlezi wa watoto. Jambo la kusikitisha ni kuwa mwanamke hapewi malipo yoyote yale ya maana kwa kufanya kazi hii kwani jamii huiona kuwa si kazi ya muhimu (Lyatuu, 2011).

4.3.2.7 Simulizi ya Mwanamke Tasa

> Palitoka mwanamke mmoja ambaye alikuwa hazai. Mumewe alikuwa akimtukana na kumpiga hata siku moja alidai arudishdie mahari aliyolipa kumwoa mwanamke huyo Mwanamke huyo aliamua kwenda kwa mganga ili azae.
>
> Alikwenda kwa Bi. Kizee mmoja ambaye alimpa dawa na kuzaa watoto watatu wa kike walioitwa Taga yaani kazi yake ni kukusanya kuni, Wita ni kuchota maji na Zimyaga kuwasha moto. Watoto hawa kila moja alitakiwa kufanya kazi yake. Watoto hawa walikuwa na kila mmoja na kazi yake. Siku moja Yule mama alikosea na kuwabadilishia kazi ndipo waligeuka joka kubwa. Joka hilo lilimmeza mama huyo.

Hadithi hii ilisimuliwa na Bw. Doto Mlolwa kutoka katika kijiji cha Igoko tarehe 07.09.2015 Saa kumi jioni. Ngano hii inapatikana katika muktadha wa nyumbani kwa sababu inasimulia maisha ya mwanamke aliyeolewa bila kupata watoto. Katika ngano hii mwananke anasawiriwa kama ifuatavyo: Kwanza kabisa ni mtu anayeolewa ili azae watoto. Kupitia hadithi hii tunamwona mwanamke anakosa

thamani kwa sababu hajazaa watoto hivyo anapigwa na kutukanwa. Pili mwanamke ni mtu anayefanya kazi za nyumbani. Tunawaona watoto wa mwanamke aliyekuwa tasa wana majukumu ya kutafuta kuni, kuchota maji na kuwasha moto. Katika ngano hii mwanamke anaonekana kupewa majukumu ya nyumbani wakati mwanaume hapewi majukumu haya. Mambo kama haya pia yanajitokeza katika maisha halisi ya jamii ya leo ambapo mwanamke akionekana tu anafanya kazi za nyumbani kama kuosha vyombo au kupika chakula hudaiwa kuwa ametawaliwa na mwanamke. Katika dunia ya leo watu wanatakiwa kusaidiana na kushirikiana katika kazi bila kujali jinsia ili kuleta maendeleo katika jamii (Msokile, 1992).

4.3.2.8 Simulizi ya Mti wa Msungwi

> Katika kijiji kimoja karibu na kisima palikuwa na mti wa ajabu ulioitwa msungwi. Mti huo uliaminika kautibu maradhi mbalimbali na kuleta baraka katika familia. Wachumaji wa matunda yale walikuwa ni wanaume tu wanawake hawakuruhusiwa. Ili kuweza kulinda uhai wa mti wale wazee waliitisha kikao na kupendekeza kuwa asiende mwanamke mmojammoja kuteka maji kwani anaweza kugusa msungwi. Hivyo wanawake walikwenda kuteka maji kwa vikundi.
> Siku moja binti mmoja alitoroka na kwenda kuchota maji peke yake na alipofika akachuma matunda akala mara mti ukaanza kuwaka moto. Wazee waliitisha kikao kutaka kumjua mharifu ni nani. Waliletwa wanawake wote wa eneo hilo na kila mmoja alipitishwa mbele na walipokuwa wanapita ndege alikuwa akiimba;
>
> *Jamani, jamani huyu si mwenyewe*
>
> Alipopita yule binti ndege alibadili wimbo na kuimba
> Jamani, jamani, mmemleta mwemewe
> Hivyo, wakambaini mhalifu wa mti huo, ndipo wakakata shauri auwawe.

Hadithi hii ilisimuliw na Bw. Thomas Stephano kutoka kijiji cha Isikizya tarehe 14.09.2015 saa kumi jioni. Ngano hii inapatikana katika muktadha wa kijijini kwa

sabbau inasimulia kisa cha msungwi ambao ni mti uliaminika kuleta Baraka na kuondoa maradhi. Wachumaji wa matunda haya walikwua ni wanaume tu, wanawake hawakuruhusiwa kabisa kuugusa. Binti mmoja alipougusa huo mti ulinyauka na kuwaka moto. Katika ngano hii mwanamke anaonekana kama chanzo cha matatizo katika jamii. Kupitia ngano hii tunaona mti unanyauka baada ya kuchumwa na mwanamke. Kitendo hiki inadhirisha kwamba mwanamke ndiye chanzo cha uharifu huo kwani asingeugusa mti huo usingenyauka.

4.3.2.9 Simulizi Mfalme Mbaya

> Palitokea Mfalme mmoja ambaye alitawala kimabavu. Siku moja aliitisha kikao na kuamuru wanawake warembo wakamatwe na kupelekwa kwake. Mfalme alichagua wanawake watano na kuwafanya kuwa wake zake. Wanawake hao waliishi kwa ushirikano vizuri kila mmoja alipika kwake na kula pamoja. Hawakurusiwa kutoka nje ya ngome. Siku moja mwanamke mmoja aliwashauri wenzake watafute dawa ya kumuua Mfalme kwani maisha yao hayakuwa mazuri na wangeweza kuuwawa wakati wowote. Wale wanawake walikubaliana bila kupinga na kumtuma mmoja wao atoroke usiku kutafuta sumu ya kumwekea Mfalme kwenye chakula. Walifanikiwa kumwekea dawa kwenye chakula usiku huo kesho yake Mfalme hakuamka alikuwa amekufa.
> Wazee waliitisha kikao kutaka kujua kuhusu kifaa cha Mfalme wake zake walihojiwa kwa zamu. Wanawake wanne walikataa lakini mmoja alikubali kuwa wao ndio wamemwua Mfalme kwa kumpa sumu. Baraza likaamua wao pia wauwawe.

Hadithi hii ilisimuliwa na Bw. Mwanaisha Ally kutoka katika kijiji cha Igoko tarehe 21.09.2015 saa kumi jioni. Ngano hii inapatika katika muktadha wa tawala za kijadi kwa sababu inasimulia utawala wa mfalme aliyetawala kimabavu na kuoa wanawake awapendao kwa nguvu.

Katika ngano hii mwanamke anasawiriwa kama ifuatavyo: kwanza kabisa mwanamke kama msaliti, tunaona usaliti unajitokeza mara mbili. Kwanza

wanawake watano wa Mfalme wanakubaliana na kufanya njama za kumwua Mfalme. Usaliti unaojitokeza katika ngano hii ni mbaya kwani unalenga mauaji ya mtu lakini pia unalenga kuleta uhuru kwa wanawake watano. Wanawake hawa waliolewa kwa nguvu za Mfalme bila hiari yao hivyo suluhisho la uhuru wao ni kumuua Mfalme. Pia mwanamke mmoja kati ya watano anaonekana kuwasaliti wenzake kwa kutoa siri kwamba wao ndio wauaji wa Mfalme. Usaliti huu unapelekea wanawake hawa wote kukamatwa na kuuwawa. Kimsingi usaliti huu unaweza ukawa mzuri kwani unafichua uovu uliofanywa na wake wa Mfalme ingawa mwanamke mmoja anawasaliti wenzake kwa kufichua siri yao.

Pili, mwanamke anasawiriwa kama asiye na maamuzi juu ya ndoa. Katika hadithi hii tunaona wanawake watano wanaolewa na Mfalme bila hiari yao. Kitendo hiki kinadhihirisha kwamba wanawake hawana maamuzi juu ya ndoa isipokuwa wanaume.

4.3.2.10 Simulizi ya Mtoto wa Mfalme

> Palitokea Mfalme mmoja ambaye alikua na watoto wawili wa kike. Moja alikuwa mrembo sana na mwingine alikuwa na chongo. Yule binti mrembo alipendwa sana na vijana wengi pale kijijini lakini Mfalme alikataa kuwa mwanawe hawezi kuolewa na mtu maskini. zimwi mmoja lilijigeuza na kuwa kijana mzuri na mwenye mali nyingi na kwenda kuchumbia kwa Mfalme. Mfalme alikubali akamwozesha binti yake shangwe na siku iliyofuata Binti Mfalme akaondoka na mumewe kwenda kijiji cha jirani na mumewe. Mdogo wake Binti Mfalme hakuruhusiwa kwenda kwa sababu alikuwa na chongo. Binti Mfalme aliondoka bila kujua kuwa mdogo wake alikwua akimfuata nyuma alipofika naye akafika. Binti Mfalme alichukia sana. Usiku ulipofika Binti Mfalme alilala chumbani na mumewe na mdogo wake akalala sebuleni.
>
> Yule mwanaume alijigeuza zimwi na kuwafata wenzake waende kula nyuma. Binti Mfalme alilala fofofo lakini mdogo wake

> alishuhudia yote. Asubuhi alimwambia dada yake lakini hakukubali. Mdogo wake aliamua kwenda kwa Bi Kizee jirani yao ambaye alimwambia kuwa dada yake ameolewa na zimwi ila ampe dawa ya kutafuna ili mazimwi yasiwaone. Usiku wa manane lile zimwi liliondoka na kuwafuata mazimwi wenzake. Binti Mdogo alimwamsha dada yake na kutafuna dawa na kupanda juu ya dari. Mazimwi yalipokuja hayakuwakuta yakaanza kuita 'Binti Mfalme! Kinyesi ikaitika bee! Wakaita tena Shemeji! Shemeji! Kinyesi kikaitika bee! Mazimwi yakasema tena 'Tuna njaa' Sauti kutoka darini ikasema 'Achama nikupe chakula' Ndipo Binti Mfalme na mdogo wake wakayapa mazimwi maji ya moto yote yakafa. Binti Mfalme akamshukuru mdogo wake na Yule Bi kizee. Waliporudi kwao wakamsilimua Mfalme mkasa na wakafanyiwa sherehe kubwa sana.

Hadithi hii ilisimuliwa na Fadhila Kaswa kutoka kijiji cha Ilalwansimba tarehe 07.09.2015 saa kumi jioni. Ngano hii inapatikana katika muktadha wa tawala za kifalme kwa sababu inasimulia maisha ya mtoto wa Mfalme. Katika ngano hii tunaelezwa kwamba Mfalme alikuwa na watoto wawili mkubwa alikuwa mrembo na mdogo alikuwa na chongo. Binti mkubwa alipendwa na wanaume wengi kutokana na urembo wake pia Mfalme hakupenda binti yake aolewe na masikini.

Katika hadithi hii anasawiriwa kama ifuatavyo: Kwanza kabisa ni pambo kwa mwanaume. Ukweli huu unathibitika pale Binti mkubwa wa Mfalme anavyofuatwa na wanaume wengi kuliko mdogo wake ambaye ana chongo. Pili, mwanamke ni mshauri. Tunamwana Bi. Kizee anawapa ushauri na dawa watoto wa Mfalme ili kuepuka kuliwa na mazimwi.

Katika ngano teule kumi ambazo ni Mama wa Kambo, Mganga wa Simba, Mjanja wa Porini, Rhoda, Baba Mbaya, Njaa Kijijini, Mwanamke Tasa, Msungwi na Mfalme mwanamke amesawiriwa kama asiye na maamuzi katika ndoa na mwili

wake, aliyekomboka kifikra, katili, mganga mwenye uwezo mkubwa, asiyeshiriki katika maamuzi ya jamii, anayefanya kazi za nyumbani tu, mshauri, anayeolewa ili amzalie mwanamume watoto, chanzo cha matatizo katika jamii.

4.4 Hitimisho

Sura hii imewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti kwa namna iliyosaidia kutimia kwa malengo mahususi ya utafiti huu. Malengo mahususi ya utafiti huu yalikuwa mawili na yote yamechambuliwa kwa pamoja kwa sababu yana uhusiano wa kimantiki. Tumeonyesha namna mwanamke anavyosawiriwa katika nyimbo teule na kisha tukaonyesha uhalisia wake kwa jamii ya leo.

SURA YA TANO

5.0 MUHTSARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha muhtasari wa sura zilizotangulia. Kila sura imeelezwa kwa ufupi ili kutoa mwanga wa matokeo ya utafiti huu. Sambamba na hayo sura hii imetoa mapendekezo yanayoweza kusaidia katika kufanya utafiti mwingine kwa wanazuoni wengine.

5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulihusu usawiri wa mwanamke katika ngano za Kinyamwezi. Sura ya kwanza inaeleza utangulizi wa jumla wa utafiti wetu. Utangulizi ni muhimu sana katika utafiti huu kwani umeeleza mambo yafuatayo: Sura imejadili usuli wa tatizo ambao unaeleza chanzo cha tatizo kuhusu usawiri wa mwnamke katika ngano za Kinyamwezi. Usuli wa tatizo unaeleza mawazo mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti na tafiti mbalimbali zinazohusiana na mada tafitiwa. Katika tamko la utafiti ambalo ndilo kiini cha utafiti huu pameelezwa kusudio hasa la utafiti, mtafiti ameeleza atafanya nini tofauti na watafiti waliotangulia.

Sura ya pili imejadili machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti. Maandiko hayo ni pamoja na yale yaliyohusu ngano kama utanzu wa fasihi simulizi na usawiri wa mwanamke katika fasihi simulizi kwa ujumla na katika ngano. Nia ya kufanya hivi ni kubainisha kile kilichokwisha fanywa na kuandikwa kuhusu mada ya utafiti na kubainisha mapengo yake.

Sura ya tatu imefafanua mbinu ambazo mtafiti amezitumia katika kukusanya data. Sura hii imeeleza mpango mzima wa utafiti kwa kueleza eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, zana za utafiti na mbinu zilizotumika kukusanya data. Sura ya nne imechambua na kuwasilisha data kwa kutumia nadharia ya Ufeministi. Uchambuzi umefanya kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Sura ya tano imetoa hitimisho, muhtasari na mapendekezo.

5.2.1 Usawiri wa Mwanamke katika Ngano Teule

Katika ngano zote 10 zilizochambuliwa imeonakana kuwa mwanamke anasawiriwa kama kiumbe ambaye ni duni mbele za mwanaume. Mwanaume ndiye anayeonekana ni kiongozi wa kila jambo na mara zote amekuwa akifanya maamuzi mbalimbali bila hata ya kumshirikisha mwanamke. Mwanamke anaonekana kuwa ni mtu wa kukaa nyumbani na kusubiri kuletewa kila kitu na mume wake. Sambamba na hilo, pia mwanamke anasawiriwa kama mtu mwenye huruma na upole na wakati huohuo akisawiriwa kuwa ni katili.

Pia, mwanamke anasawiriwa kama mwanamapinduzi ambaye anafanya harakati kadha wa kadha kwa lengo la kujikomboa. Hili lilitokea pale ambapo mwanamke ameshindwa kuvumilia madhila ya mumewe ya kumtaka kukaa ndani muda wote bila ya kufanya kazi na yeye mwanaume akiweka mkazo zaidi wa kutoa fedha za matumizi kwa mke mdogo peke yake. Pia, mwanamke anasawiriwa kama mtu ambaye ana chuki dhidi ya wataoto wa mke mwenzake ambapo anaonekana akifanya hila ya kuhakikisha watoto wa mke mwenza wanakatishwa uhai wao wa kuishi hapa duniani.

5.2.2 Uhalisia wa Usawiri wa Mwanamke katika Ngano Teule

Matokeo ya utafiti yamethibitisha kuwa katika ngano teule usawiri wa mwanamke umejaa uhalisia kwani mambo yote aliyosawiriwa nayo yanatokea katika ulimwengu halisi. Ni kweli katika jamii ya leo ya Wanyamwezi na nyinginezo wapo baadhi ya wanawake ambao ni katili dhidi ya watoto wa wake wenzao maarufu kwa jina la watoto wa kambo. Baadhi ya wanawake hao hufanya ukatili uliopitiliza na hata kumuua mtoto wa kambo. Hii ni hulka inayotokana na mtu mwenyewe vile anavyomchukulia mtoto wa kambo. Hata hivyo wapo wanawake wengi tu katika jamii ambao wana mapenzi ya dhati kwa watoto wa kambo. Hawa wanafaa kuigwa na wale wanaowatesa watoto wa kambo wanatakiwa kupigwa vita kwa kufichuliwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria. Suala la kwamba mwanamke ni mlezi wa familia, halina mjadala kwani ni kweli tupu kwamba wanawake ndio walezi wakuu wa watoto na hili linajitokeza katika maisha halisi ya jamii.

5.3 Utoshelevu wa Nadharia

Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni nadharia ya Kifeministi. Kwa vile nadharia hii hutumika kuchambua matini kwa kuangalia mahusiano ya mwanamke na jamii yake, hivyo nadharia hii ilitumika katika kuangalia namna mwanamke alivyosawiriwa kwa kuangazia masuala ya kijamii, kisiasa na kijuchumi ubaini namna mwanamke alivyosawiriwa katika ngano za Wanywezi.

5.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulilenga kuchunguza nafasi ya mwanamke katika ngano za Kinyamwezi. Baada ya kufanya uchunguzi na kupata mahitimisho utafiti huu unatoa mapendekezo

kwa jamii na kwa tafiti zijazo kam aifuatvyo:

5.4.1 Mapendekezo kwa Tafiti za Baadaye

Fasihi Simulizi ni pana sana. Katika utafiti huu tumeangalia kipengele cha fani hususani mhusika mwanamke. Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza namna mwanamke anavyosawiriwa katika ngano za Kinyamwezi. Kuna wahusika wengine ambao utafiti huu uligundua wahusika hawa ni wahusika wanaume, wahusika mazimwi pia wahusika Bibi Kizee. Wahusika hawa bado hawajafanyiwa uchunguzi katika ngano za Wanyamwezi hivyo tafiti zijazo zinaweza kufanya uchunguzi kwa wahusika hawa.

Aidha utafiti huu uligundua katika ngano za Kinyamwezi kuna matumizi ya nyimbo. Nyimbo ni kipengele cha fani ambacho ngano kina dhima mbalimbali. Tafiti zijazo zinaweza kukiangalia kipengele hiki. Utafiti huu unapendekezwa kuwa tafiti zingine kutumia nadharia nyingine katika kuchunguza usawiri wa mwanamke ili kupata matokeo tofauti.

5.5 Hitimisho

Matokeo ya utafiti huu yanahitimisha kwamba ngano za Kinyamwezi zinasawiri hali halisi ya maisha ya mwanamke katika jamii ya Tanzania. Nafasi nyingi alizopewa mwanamke ni duni na ambazo zimelenga kusawiri hali halisi ya mwanamke ya jamii ya Wanyamwezi.

MAREJELEO

Balisidya, M. L (1982). "The image of Women in Tanzania Oral Literature" *Jarida la Tuki*, 49(2), 8-21.

Chiraka, P. (2002), "Nafasi ya Mwanamke katika Nyimbo za Harusi za Kabila la Wajita," Tasinifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Tanzania.

Finnegan, R. (1977). *Oral Poetry its nature, Significance and Social Context.* Cambridge: Cambridge University Press.

Kabeya, J. B. (1966). *Watu Mashuhuri wa Tanzania: Mtemi Mirambo,* Kampala: East African Literature Bureau.

Kipkorir, S. (2004). Nafasi ya Mwanamke katika Methali za Abakuria. Utafiti wa Fasihi Simulizi, Chuo Kikuu, Dar es Salaam, Tanzania.

Kitundu, N. J. (2012). Usawiri wa wahusika Wanawake katika Ngano za Wanyiramba. Tasnifu ya M. A. Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Koda, B. (2000) "The Gender Dimension of Land Rights in Tanzania: Case Study of Msindo Village, Same District", Unpublished *Ph.D Thesis*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Kothari, C. P. (2004). *Research Methodology, Methods, Methods Techniques.* (2nd ed). New Delhi: New Age International Publishing Limited.

Mackinnon, C. A. (1991). *Towards A Feminism Theory of the State.* London: Havard University Press.

Madsen, D. L. (2000). *Feminist Theory and Literary Practice.* New York: Phot Press.

McDowell, L. (2003). *Place and Space* in *A Concise Companion to Feminist Theory*, London: London University Press.

Mnenuka, A. (2011). *"*Taswira ya Mwanamke katika Muziku wa Bongo Fleva: Mifano kutoka nyimbo Teule," katika *Mulika*. na 29 & 30 uk 69-87, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: DUP.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* TUKI: Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1999). "Utenzi wa Mwanakupona." Katika *Tenzi Tatu za Kale*. Uk 127-130, Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mwamanda, F. (2001). "Utafiti juu ya Nyimbo za Kinyamwezi." Tasinifu ya Shahada ya Kwanza, Chuu Kikuu Dar es Salaam.

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature.* Bloongton: Indiana University Press.

Omari, S. (2011). "Taswira ya Mwanamke katika Muziki wa Bongoflava." Mifano kutoka katika Nyimbo Teule, katika *Mulika,* Na 29&30, uk 69-83, Dar es Salaam: TUKI.

Ramadhani, S. K. (2013), "Usawiri wa Mwanamke Katika Taarab ya Mipasho: Mfano Kutoka Nyimbo za Mzee Yussuf Mzee". Tasinifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Richard, M. (2002). "Fani na Maudhui ya Methali katika Jamii ya Wanyamwezi." Tasnifu ya kumaliza Shahada ya kwanza, Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi, Mfululizo wa Lugha na Fasihi: Kitabu cha Kwanza.* Dar es Salaam: KAUTU.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake.* Nairobi: Phonex Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Limited.

Wamitila, K.W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications.

Wanjala, F. S. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi, kwa shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Bookshop.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Na. 1: Masimulizi ya Ngano Teule za Kinyamwezi kwa Lugha ya Kinyamwezi

Simulizi ya Mke wa Mwa Bhabha

Kale kakawuka!
Kuwukilage wuleko!
Aho siku zya kunuma pafumilage Tununonere. Tunononere wali nsabhi wa ng'ombe wali na wakima bhabhili lakini yumo mhanya akaja kukaya yawo. Oshinga nkima yumo akabyala wana bhabhili. Nkima mhanya waja akaleka mwana omo mngosha. Lushiku lumo mkima mdo akamwila mwana wakwe aje akadime kamakomkima mhanya.

Aho waja kukadima kozimija ng'ombe kadya kuzichora, kosangana na kagikulu kamo. Kagikulu kyoyomba "Olizahe mwizukuru wane? Koyomba 'nazimizyaga ng'ombe zyane'. Kagikulu komuwila nilambage lilonda lyane olowamala kulilamba kilonda kitula ngumi. Aho walamba, wakitula ngumi kofumila kawa kado kado. Oyo bibi omwila mfatage mnambwa mwenoyo okozipandeka ing'ombe zyako. Aho wandya kuja akawa kundya kumuhya harufu ya ing'ombe mpaka kozipandika.

Aho wazipandika ing'ombe washoka kaya, akasika obhuziku akasika olugirila jing'ombe. Aho yashika ndiyu obhabha wake omwila hangi kadimage ing'ombe. Oyo nyanda aho waja kukadima akaleka kawa kukaya. Ninando wandya kowawela abhana bhakwe 'onene nalemaga okwikala na onyanda nalekowa namtulile wuganga kuwugali mkamuwile.

Aho wafuma ukadima olugarila ing'ombe. Mnambwa wale wa maajabu, hadoo womfuata munyanda ogwo omwila 'owo ugali wakulekelaga okawule uli na uganga. Mnyanda wenoyo oleka kulya walala.
Kamgani kane kamalila enenho!

Mufumu wa Nsimba
Kamgani! Kamgani!
Kakawukila wuliko
Akale zyali zyiho ndimu zikalage hakimo. Lusiku lumo Nsimba yuyombaga ndimu nzehe zidime. Kamnasayaye kakatogilwe mihayo yayomba Nsimba kumvisa gukuye mwipilinga, kukumfilila chakulya na minzi kila siku.

Lusiku lumo Nsimba yali yalalile yuleka mlomo wazi. Nzoka yafikiri mulomo genugo ipilinga. Yuwingila mgati mwa mlomo gwa Nsimba. Nsimba aho yatunura yuwingwa muda mwatimba sana uwitana wafumu wose wumpa lakini akapilile. Kamnasayaye komuwila Nsmba gukuye mfumu mhanya sana, uwongeza gukuye nawe mnampala

aliwagoha kudimwa. Nsimba yatogwa sana nalikwahidi kuwa akidudimwa. Akumpa zawadi.

Gukuye na Mnasayaye uwitanwa uzumya kuyilagula Nsimba. Uya mwipori ukadima ngoso, uyifila ambele ya mlomo gwa Nsimba. Uyiwila Nsimba asamaga mulimo, uyitulila ngoso bihi na mlomo gwa Nsimba. Gukuye na Mnasayaye uyifuma ngoso na ngoso yulila.. nzoka aho yigwa muzwi gwa ngoso yufuma muna haraka. Gukuye Mnasayaye uyilekea ngoso, ngoso nayo yupela.

Nzoka yumpezya ngoso. Nsimba yawa yapilile kabisa. Nsimba baad aya kupila yumpa zawadi nsoga sana gukuye na Mnasayaye.

Simulizi ya Mpulungu wa Mwipoli
Kale kawuka !
Kawukilage wuleko !

Akale ni ka gwanota sana ndimu zya mwipori zyabhona minze ndoho kabisa. Ndimu zininzyo zyali Mnaluung'ando, Mbiti, Nsimba, Nhorongo, Nguku, Nhinga, Mpulu na bhandi kiti Mnadongo. Mtemi wawo wali Mnampuli wuyomba bhagosha ! Bhagosha Tehelezye mkutano.

Lushiku lwa lushiku Mtemi na msaidizi wakwe wakikuminga hakimu kulola mattizo ago galisumbua mlikijiji lyabho. Mtemi ukoma na kufungula kakao woyomba 'ndibhakaribhishe wose bhana nzengo kulola matatizo ago galisumbula mnzenfo gwise gunugu. Ilengo twite kinehe kuinja itatizo lay minze mwieneo liswe limili. Ndibhakribhishe kusangalia mawazo twite kinehe'.

Mnansimba uyomb "Mtemi nene nalifikiri kuenja itatizo linili tusembe lwinzi'. Ndimu zyose zyutula kufurahia liwazo linilo. Kanyaga kuwita hadoo ugorola mkono Mnamg'ando wuyomba nane nalimuunga mkono mnamala Mnansiomba. Ugorola hange mkono Mhahorongo na kuyomaba 'mawazo ga hbose galifaya sana kwo pande ndoho shida ndi yatari kusimba lwinzi lwenulo lakini kwe na kagoro, kagoro kenako luluhusu inswe tuki na mundu na nonga tukwita kinehe? Bhose bhohaya 'tukusimbila mbembe ziswe'.

Lushiku lwa lushiku wose woikuminga na kuandya kusimba lwinzi Mnamg'ando akasikile. Wangi wose wandya kusimba na womala, wakasimbila siku idatu. Minzi gowi mingi wokame wokugaya. Lakini kila lushiku minzi guwi guchafuka. Mtemi uwakuminga hangi wananzengo kulola itatizo linilo. Mtemi uyomba 'mkutano gunugu gutujaduiliwaga henaha ndikowa kuwina milimo gunuhu katika makundi awili; ndimu zya mpembe na ndimu zya izyozigale mbembe umgundua nani adui wiswe.

Zamu zyunda na Simba, lung;ando ipita nili buyu lya bhuki wumtunga Nsimba kumti halafu wumleka. Wiza hangi kobekobe akafanikiwa kumdima mng'ando aho mkala wiza wose woikuminga kumhoji.
Na mgani gwani kushila.

Simulizi ya Rhoda

Kale kakawuka!
Kawukilage wuleko!
Enaho kale wale alewo bhabha yumo na mayo yumo bhikala mnyaka minge bhila kubhyala. Kwimanela Mungu bhobyala mwnaa vumo Rhoda. Uyo bhabha akazikile na mwana yumo obhona akatoshije, otola hange mkima wa kabhili.
Obhyala wana wawili.

Lusiika lumo umkoma mhanya oja kukelelo. Woja wana wa mkima mdo bhoziku ko ha Rhoda, woyomba Rhoda tujage kong'wi. Rhoda woyomba nne natekuja lelo nena melemo nakoja eigolo. Lusiku lwa kabili wowita hange, Rhoda tujage komakwi. Rhoda woyomba nenen natekoja. Lusiku lwa kadatu hange womuwela Rhoda tujage kumakwi. Rhoda uzumya woja kumakwi. Aho wosika womuwela Rhoda jelage nkwi yeyokwo, Rhoda woisoka aho woisola odumbekela mwisimo. Aho wadumbekela wakamfulela aho wamala kumfulela wotunga miligo ya nkwi woja kaya. Aho wosika kaya mayo wa Rhoda wo uwawoja Mwana wane Rhoda mwamlekaga hale? Woyomba wali aleyomba uliwahi kuja imawe.

Muda si mlihu koja kayayo komakwi osika aandya kusenya makwi. Owimanela mwana alemba mwisimo.

Ewi bibi mtondolankiwi tandago olomo.
Lubhili kamwelage bhabha na mayo wamefulelaga mwisimo.

Yule ngikulu aho wamala oja okawawela bhabha na mayo wa Rhoda, woja wokamfulola kunu nina wo ng'wana Rhoda alelela kunu alemba.

Mwana wane bhanibhulilaga,
Mwana wane Rhoda nakalai mhona hange.

Kuno bhabha wakwe awasemba mpka wosika kumwisho, songa nzoka mhanya sana wa kusangaza kwimanela nziko yomluma bhabha Rhoda ni shimo lyoifulela.

Simulizi ya Bhabha Mbhi

Kamgani ! Kangani !
Bhale bhafumile bhabha umo na mayo umo bhale bhekala chisoga sana. Babhyazi blenabha bhakabhyala wana wakikima wadatu. Lusiku lumo bhakabhuka bhana na ninabho mwipori kukasenya nkwi. Hado itungo ido ikafumila Nsimba na kubhopezya aho bhandya kupela mwana umo akadimwa na Nsimba. Mayo mwenoyo na bhana bhakwe bhabhili bhosubha kukaya.

Aho bhasika akaya mgosi wakwe wambhuzya mke wake 'Mwana wani yungi wamlekahe' ? mke wakwe wayomba 'Wadimagwa na Nsimba'. Katungo mgosi wakwe wampezya mke wakwe wasiga na bhana bhakwe bhabhili.

Wikala mwaka gumo wandya kubhatogwa bhana bhakwe, wandya kubhatola. Bhana bhenabho bhaleka kuitogwa sembo ya mwansamho. Lusiku lumo hbomuwila mayo omo wa kigikuru, omayo mwenoyo akawawile bhamfile kubhanu bhahanya

bhakamshitaki. Aho bhamfila kubhanikule asame msi yeneyo kunguno walete kuponda nsoni mchalo chenecho.
Namala kamgani kane.

Simulizi ya Nzala ya Mchalo
Mchalo chenecho akafumila nzala hanya sana. Mtemi Milambo na mgana gwakwe gose lyale nzala hanya sana. Kila lwisi Milambo akaja mchalo kinge kukobha chakulya. Milambo wabhaga na nsembo ya bhutubhu. Kila lwisi watetaga. Mke wa Milambo wabhage otabhaniwe bhufuma obho wasigage wala akabhubhonaga. Wambhuza mgosi wakwe wakilwa mno.

Lusiku lumo mke wa Milambo wayomba akale kulala tulo na kwilabhila, wakobhaga ammanye mwibhi wa bhufuma. Bhuziko aho wingila wombhona mgosi wakwe wabhoka wandya kuzuga bhugale. Mke wakwe watunula na kumuwila mgosi akwe 'Okubhagi ulya winene? Milambo wakimwa mno wabhona amabhanga gakwe wantula mkw wakwe.

Simulizi ya Mkima Mgumba
Kafumile mkina wale akabhyalaga. Mgosi wakwe wamdudake na kumtula. Lusiku lumo wakobhage wamsubhizye ensabho zyake ezyo wafumya kumtola mke wakwe. Mkima wenoyo wabhoka kuja kumfumu kukakobha bhubhyazi.

Mfumo wenoyo wampa bhuganga wabhyala bhana bhadatu wabhita Taga yaani kusenya nkwi, Wita yaani kudaha mizne na Zimyaga yaani zimaga moto. Mfumu wampa miiko, kila mwana atumame mlimo gwake. Taga kusenya nkwi, wita adahe mizni na Zimyag apembe moto.

Bhana bhenabho bhakakula kila mwene watumamage mlimo gwake. Lusiku lumo mayo wenoyo wale lababhila wobhapa muhimu hunhi. Ahene abhana bhenabho bhogaluka bhobhi nzoka mhanya. Inzoka yeneyo yammila mkoma mwinuyo.

Simulizi ya Msungwi
Chalo kimo akafumila mti mhanya bihi na lwinzi gwitanagwa msungwi. Mti gwenogo bhale bhagutogwa kunguno gwaletage chelu kubhanu. Abho bhaya bhage msungwi ngwenugo bhabhage bhagosha duhu, bhakina bhale bhabhakanila.

Bhamnampala bhali bhitana bhantu bhikale kasumbi bhikale kugulinda mti gunugwo. Bhakayomba mkima umo umo akaje kudaha mizne. Mwineyo akobholule kiduma msungwi kuhege bhakima bhale bhaja bhingi kudaha minze.

Lusiku lumo mwaniki umo akabhoka kukadaha mizne inene. Aho wasika amti gwenugo wayabha msungwi gwenugo. Aho wayabha mti gwandya kubhaka moto. Wanyampala bhoikala akasumbui kumana nani wakenga msungwi gwenugo.

Bitanwa bhakima bhose bha mchalo kila yumo bhambhitazya ambele. Aho bhabhitage noni yowanda kwimba lwimbo.

Makene meneg, makene nenge, mwaleta yungi.
Aho wabhitaga mwaniki mwenuyo wakenaga noni akimba lwimbo lwingi.

Makene, makene nenge mwaleta mwekili.
Kehene bhamanya oyo wakenaga mti gwenugo.

Simulizi ya Mtemi Mbhi

Akafumila mtemi umo mbhi. Lusiku lumo akabhita na bhanampala bhabhadime bhakima bhasoga bhamfilile kukaya yakwe. Mtemi wusagula bhakima bhatano na kubhabhezya bhabhe bhakima bhakwe. Bhakima bhenabho bhakile sisoga bhayokutumanila akimo. Kila mwene wadekake mkaya yakwe bhulya hakimo. Bhabhahakanzya kufuma mnomwa.

Lusiku lumo mkima yumo ale awawila bhiye bhakobhe bhuganga bwakumbhulaga mgosi wabho kunguno kikale chabho chale kikabhile kisoga. Mtemi wale akobholile kubhabhulaga itungo lyose bhakima bhenabho bhakakanile. Womtuma umo akakobhe bhuganga bhokumtulila Mtemi. Kubhamtulila bhuganga mtemi mwenuyo akabhukile, wafya.

Bhanampala bhowitana bhampala bhicacho bhamanye eke chambhulaga Mtemio. Bhake bha Mtemi bhabha bhogazye yumo yumo. Bhakima bhane bhabhe bhale bhakana lakini mkima yumo wazyumya kitisi bhambhulaga Mtemi. Libhanza lyazyumya libhabhulage.

Simulizi ya Mwana wa Mtemi

Wale wafumile mtemi wabhaga na bhana bhabhili bha kikima. Umo wabhaga msoga mmno na yungi wabhage na nsongo. Omwaniki mwenuyo msoga wale wakamtongwa mno bhayanda bha mchalo chenicho. Mtemi akakana mwana wake aleke kutolwa na mduki.

Izimwi limo lyowigalula obhi msumba msoga lwoya kukakobha bhutozi kumtemi. Mtemi akazumya akamtozya mwana wakwe. Lusiku lwa kabhili akabhoka na mgosi wakwe kuya mchalo cha jirani yakwe. Nsongo bhamkanile kuya na mkulywe kunguno ali na nsongo.. mwana wa Mtemi akabhuka kuya akamanikizye kitisi nzunaye alemlonda kunuma. Ulubhalesika nawe wosika. Bhuzika bhakalalal kumbele na mgosi wakwe mzunaye wolala asebule.

Izimwi linelyo bhaduguze bhiza bhalye nyama. Mkuluye Nsongo wale walala tulo nyingi ningi lakini mzunaye akalalile akagowona gopse. Diyu wamuwila nkuluye gose wakana kuzumya. Mzunaye akabhoka kukambhuzya Mgikulu yumo. Mgikulu mwinuyo wayomba nzunayo watolwa na zimwingla nokupa waganga bhukabhezye lileke kubhabhulaga Mgikulu mwinuyo wampa wuganga wa kudakuna ole gize bhuziku gakabhabhulage.

Bhuziku bhikingilima lizimwi lyenelo likabhoka kubhalonda ndiye Nsongo wamumisha mkuluye wadakule uganga na kulina kukanu. Mazimwingala aho gioza bhakabhasangile. Gyanda kuitana Bhebhe mwana wa Mtemi! Mafi getabhuka alam! Mkwela wane! Hangi mafi getabhuka lama! Mazimwingala goyomba. "Tuli na nzala"! baliyomba kukanu "Wasama mlomi akupe chakulya"! mazimwingal gasama mlomo kughene mzunaye na Mwana wa Mtemi bhabhapa minzi ga moto, gose gofwa. Wamana wa Mtemi wamlumba sana m,zunaye na mwenuyo mgikuru. Aho bhasubha kukaya bhamuwisha Mtemi na Mtemi akabhabhezezya sherehe ihanya mno.

KIAMBATANISHO NA. 2: Hojaji kwa Watafitiwa

Hojaji hii inalenga kubainisha usawiwi wa mwanamke katika ngano za Kinyamwezi. Tafadhali ninaomba ujibu maswali yafuatayo kwa kadri unavyoelewa. Majibu yatakayopatikana ni kwa madhumuni ya utafiti huu tu na si vinginevyo.

Taarifa Binafsi

1. Jina lako……..……
2. Umri……
3. Kabila lako……
4. Kijiji unachoishi……
5. Je, umeishi katika eneo hili kwa muda gani?.....

Katika sehemu ifuatayo weka alama ya (√) mahali panapohusika.

6. Jinsi: Ke ( ), Me ( )
7. Hali ya ndoa: umeoa/ kuolewa; ndiyo ( ), hapana ( ): hujaoa/ kuolewa; Ndiyo ( ), hapana ( ): mmetengana; ndiyo ( ), hapana ( )
8. Kiwnago cha Eliu: msingi ( ), Sekondari ( ), Chuo ( ), Hakun ( )
9. Lugha unayozungumza: Kinyamwezi ( ), Kiswahili ( ), Kingerez ( ) Lugha nyingine ( )
10. Kazi yako……..……

Taarifa kuhusu nafasi ya mwanamke katika mgawanyo wa majukumu kijinsia katika ngano za Kinyamwezi

11. Je, unafahamu ngano yoyote ya Kinyamwezi? Ndiyo ( ), Hapana ( )

12. Je, ngano hiyo inamzungumzia usawiri wa mwanamke? Ndiyo( ), Hapana( )
13. Kutokana na ngano hiyo uliyoisimulia, je mwanamke anaongelewa vipi?
14. Unafikiri kwanini mwanamke ameongelewa hivyo katika ngano uliyosimulia?
15. Kulingana na hadithi uliyosimulia kuna uhalisia gani kati ya mwanamke katika ngano hiyo na mwanamke katika jamii ya Wanyamwezi?

Ahsante kwa mawazo na ushirikiano wako